

**LAPORTA ATAKA XAVI ABAKI BARCELONA**

UKURASA 22

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumanne Machi 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581627
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Utata waibuka sheria kukiukwa

UKURASA 2




Gavana wa Benki Kuu, Emmanuel Tutuba.

Illustration, graphics: binharun79@gmail.com

## Wakazi Msimbazi kulamba bil. 52/- kuhama bondeni

UKURASA 19

MAKALA MAALUM

Mjane mdogo zaidi arejeshwa shuleni, yuko darasa la VI, ana watoto 2

UKURASA 4



**Gari** la kifahari lenye bendera ya chama lanaswa lina wahamiaji haramu 20

UKURASA 5



**Kumekucha** Ripoti ya CAG ikitua kwa Rais Samia wiki hii

UKURASA 7



## Mbowe: Tunarejesha heshima CHADEMA 2024 na 2025

UKURASA 19

**MICHEZO** PACOME, AUCHO FITI KUIVAA MAMELODI UK.24 **KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akioneshwa na Mwanafunzi wa kidato cha sita wa shule ya wasichana ya Msalato, Rosemary Brighton namna wanavyofanya mafunzo kwa vitendo ya upasuaji, wakati wa mkutano wa wadau wa elimu mkoa wa Dodoma kwenye ukumbi wa Chuo cha Biblia mkoani Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

TOZO ZA UTALII

# Utata waibuka sheria kukiukwa

**Na Mwandishi Wetu**

UTATA umeibuka wafanyabiashara kuilalamikia serikali, ikiwamo Wizara ya Maliasili na Utalii, kutoza wateja wake kwa Dola, ilhali kuna maagizo matatu ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kukemea ukiukwaji huo unaokinzana na sheria yake ya mwaka 2006.

Tangazo la BoT la Juni 20, mwaka jana, lilielekeza, "Benki Kuu inapenda kuukumbusha umma kuwa kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006 kinaelekeza kuwa Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha pekee ambayo inaruhusiwa kutumika nchini.

"Hivyo, hakuna mtu au kampuni yoyote inayoruhusiwa kuikataa kwa malipo yoyote halali (legal tender). Kitendo cha kukataa malipo kwa Shilingi ya Tanzania ni kuvunja Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006."

BoT katika kikao chake cha kupata maoni ya wamiliki wa hoteli za kitalii jijini Arusha hivi karibuni kuwa na maduka ya kubadilishia fedha kwenye hoteli zao, Mwenyekiti wa Chama cha Wakala wa Utalii (TATO), Wilbard Chambulo, alilalamika wanalazimishwa kutumia Dola, hatua inayowasababishia hasara na magumu kibiashara.

Akashauri matumizi holela ya Dola nchini yadhibitiwe kwa kuwekwa mifumo thabiti, ikiwamo kiwango sawa cha kubadilisha fedha, huku wakilia kuwapo utitiri wa tozo zinazolipwa kwa fedha za kigeni, akitaja mifano ya leseni za madereva wa magari ya utalii.

BoT katika tangazo lake hilo la miezi tisa iliyopita, ilikumbusha kuwa ni mara ya tatu, likitanguliwa na mengine ya Agosti 2007 na Desemba 2017, ikafafanua:

"Katika siku za karibuni imebainika kuwapo ukiukwaji wa tamko hilo. Hivyo, Benki Kuu inapenda kuukumbusha umma kwamba maagizo yaliyotolewa hapo awali kuhusu matumizi ya fedha za kigeni yanapaswa kuendelea kuzingatiwa kama ifuatavyo:

" Bei zote hapa nchini zitangazwe kwa Shilingi ya Tanzania. Bei hizi zinajumuisha kodi za kupangisha ardhi, nyumba na ofisi; gharama za elimu; huduma za afya, vifaa tiba na vitendanishi; gharama za usafiri, lojistiki na bandari; vifaa vya kielektroniki na huduma za mitandao ya mawasiliano.

"Bei ambazo walengwa wake wakuu ni watalii au wateja wasio wakazi zinaweza kutangazwa kwa fedha za kigeni na malipo yake yanaweza kufanyika kwa fedha za kigeni. Bei hizi zinajumuisha gharama za hoteli, usafiri, gharama za viwanja vya ndege na viza kwa wageni, usafirishaji kwenda nchi za nje kupitia Tanzania na gharama za mizigo bandarini.

"Walipaji wanaotumia fedha za kigeni watambuliwe kwa vitambulisho vyao kama pasi za kusafiria na nyaraka za usajili kwa kampuni.

"Viwango vya kubadilisha fedha vitakavyotumika katika kuweka bei hizo viwekwe wazi na visizidi vile vya soko. Ifahamike wazi kuwa ni benki na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni pekee yanayoruhusiwa kupanga viwango vya kubadilisha fedha kutokana na ushindani katika soko la fedha za kigeni.

"Mkazi yeyote wa Tanzania anapaswa kufanya malipo kwa kutumia Shilingi ya Tanzania pekee na hivyo asilazimishwe kulipia bidhaa au huduma yoyote nchini kwa kutumia fedha za kigeni."

Mwenyekiti wa TATO, Chambulo, alishauri BoT kupitia upya utaratibu wa matumizi ya Dola nchini kwa kuhakikisha wageni hawatumii sarafu hiyo wakiwa nchini, bali watumie kadi na mifumo ya kibenki ili serikali izione.

"Wewe nipe shilingi sina shida, ila usinipe Shilingi halafu benki fulani alipe kiwango cha kubadilisha cha Sh. 2,500, duka la kubadili fedha anipe Sh. 2,700 na benki nyingine anipe Sh. 2,000. 'There is no control' (hakuna udhibiti).

"BoT chukua Dola juujuu (kwenye mfumo), wewe tupe Shilingi, siyo kila mtu anakuwa na kiwango chake cha kubadilishia fedha, inasababisha tunapata hasara kwenye kubadilisha fedha hizo," alilalama.

Alisema ni vyema kujifunza Afrika Kusini ambako hawana rukhsa kubadilisha Dola mtaani.

"Ni kwanini serikali yetu taasisi zake ndio watumiaji wakubwa wa Dola? Hazina leseni ya kubadilisha Dola kwa sababu wao ndio wanaopokea Dola. Ukishachukua Dola, unamchaji mzungu Dola ambazo ukishaziingiza nchini unatumia benki. Mzungu hawezi kuja na Dola milioni 27 taslimu. Najua BoT mnaziona kwenye mifumo yenu.

"Zikiingia benki, BoT mnaziona, nikianza kuzitumia kila mmoja (taasisi) anazitaka, ndio sababu mmekosa Dola. Kodi hatuna, shida nayo tunalipa kwa Shilingi lakini tozo zinatuumiza.

TANAPA anataka, Serengeti, Ngorongoro, Wizara ya Maliasili na Utalii ndio inaongoza kwa tozo. Mimi ninalipa tozo za sekta ya utalii Dola 157,000, wanakupa kiwango cha kubadilishia kwa Dola, hawataki Shilingi.

"Juzi wamekuja Mamlaka ya Usafiri Ardhini (LATRA) wamesema wanataka Dola, sasa sijui wanaona sisi tunazitengeneza? Kila taasisi ya umma inataka Dola kutoka kwetu.

"Chukueni hizo Dola, ninyi tupeni fedha za Kitanzania lakini kwa bei ya kubadilishia yenye usawa na si kama hali ilivyo sasa kila mtu ana bei yake," alishauri.

Mwenyekiti Chambulo alisema hakuna mgeni anayebadilisha fedha za kigeni hotelini kwa kuwa huko inabadilishwa kwa gharama ndogo sana, badala yake wanapelekwa mtaani na wanapokuja kununua kinywaji hotelini, wanataka walipe kwa Shilingi na ndio chanzo cha hoteli kutaka Dola kwa kuwa kote kwenye mamlaka wamiliki wa hoteli wanalazimishwa walipe tozo kwa Dola.

Alishauri serikali ifanye utafiti kujua ni kiasi gani cha fedha za kigeni mtalii anatumia ndani ya hoteli kwa muda anaokuwamo hotelini ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu na mgeni alazimishwe kupitisha benki au kadi ili Dola zionekane kwenye mfumo.

"Hizi taslimu ni tatizo, mturuhusu tuweke matangazo kwamba hatupokei fedha za kigeni, lakini ukiniambia nikiuza chai niuze kwa Shilingi, ni lazima kumwuzia mswahili... zamani kulikuwa na fomu maalum ya mgeni kueleza kiwango cha fedha za kigeni alichoingia na nacho nchini.

"Zamani ilikuwa mtalii akiingia Mount Meru Hotel walikuwa wana leseni ya kubadilishia fedha na ilikuwa inagongwa muhuri kwamba ametumia kiasi gani na wanaangalia alichotumia.

"Tatizo lipo, taasisi za serikali hawataki Shilingi kabisa, Ngorongoro na kwingine wanakutoza Dola. Tunapata tabu sana Mungu atatusikia na Mama (Rais Samia Suluhu Hassan) atatusikia.

"Zikiingia Dola benki wanakata,ukiingia ndani ya geti la chuma la Serengeti wanataka Dola 130, mwingine ameweka kamba tu wanatoza Dola, unapewa risiti ya Shilingi kwa kiwango cha Sh. 2,200 ambacho wameamua wao hakipo BoT wala kokote, wamepanga wao, tutalalamika kwa nani? Tumenyamaza.

"Wizara ya Maliasili na Utalii hujapeleka Dola Januari, huruhusiwi kuingia kwenye hifadhi yoyote, tunalipa Dola 10,000 hadi 20,000 ambazo hata maduka ya kubadilishia fedha hawalipi hiyo licha ya kwamba wanafanyabishara ya mabilioni. Leseni ya madereva wa utalii ni Dola 50, kama huna hupewi.

"Tunaomba msafishe kwanza nyumba kule ndani, ndipo mje kwetu wapigakura (shughuli za utalii). Lakini tukubaliane nikishaingiza Dola ukazichukua ni muhimu ninapozihitaji kama kununua gari nizipate kwa sababu ununuzi wote tunafanya kwa Dola," alisema.

Ni kauli ya wadau hao iliyotoka baada ya BoT kuelekeza hoteli zote za nyota tatu hadi tano nchini kuwa na leseni za maduka ya kubadilishia fedha za kigeni ifikapo Julai Mosi, mwaka huu.

BoT iliwaita wamiliki wa hoteli za kitalii jijini Arusha kutaka kupata maoni yao kuhusu maduka hayo ya kubadilishia fedha kwenye hoteli zao.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba alisema watalii wanakuja na fedha za kigeni; serikali imegundua kwenye hoteli wanazipokea na kuziuza kwenye soko haramu.

"Sheria inasema huwezi kuruhusiwa kufanya miamala ya kubadilisha fedha za kigeni kuja Shilingi kama hauna leseni. Kwa misingi hiyo, nikaona tukutane tujadili lakini sisi kwa nafasi yetu tuliamua kuboresha kwa kufungua fursa kwa wamiliki waweze kumiliki na kuendesha maduka ya kubadilishia fedha.

"Kwa kufanya hivyo, tunaamini tutakuwa tumeboresha huduma za utalii na tatizo la wageni kukosa fedha za kigeni na kuibiwa wanapokwenda kutafuta kubadilisha. Lengo tuendelee kuboresha mazingira ya biashara kwenye sekta hii," alisema.

Gavana Tutuba alisema tangu kutungwa kwa kanuni za jambo hilo, kwa Dar es Salaam ni hoteli moja pekee ilikubali kufanya hivyo, huku Zanzibar na Arusha hakuna hata moja.

Alisema leseni haitakuwa na gharama yoyote ya mtaji na kwamba dhamira ni kurahisisha mazingira ya biashara ili kuwe na weledi, uhuru na uzingatiaji sheria.

Kwa mujibu wa Tutuba, nchi ina benki 37 zenye matawi zaidi 900 na maduka ya kubadilishia fedha 18 yenye matawi 96, lakini idadi hiyo haitoshi, hali inayosababisha watalii kukosa huduma.

"Kuuza dola kwenye black market ni uhujumu uchumi, sheria imetoa adhabu ya Dola 3,000 kwa kosa au kukupeleka mahakamani," alisema.

Juni mwaka jana, BoT ilitoa taarifa kwa umma ikikumbusha wananchi kuhusu katazo la matumizi ya fedha za kigeni kwa wakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kulipia bidhaa na huduma nchini, baada ya kubaini ukiukwaji wa tamko la Agosti 2007 na la pili la Desemba 2017 kuhusu jambo hilo.

Hivyo, kitendo cha taasisi za serikali kukataa malipo kwa Shilingi ya Tanzania ni kuvunja Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwaka 2006.

TANGAZO


Nipashe
MWANGA WA JAMII
Tunaendelea kuhesabia siku...
Kaa Tayari kupokea Jambo Jipya
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com

MAKALA MAALUM

# Mjane mwenye umri mdogo zaidi nchini arejeshwa shule

## •Aliozwa akiwa na umri wa miaka 11
## •Wajane wajitosa, sasa yuko la VI



**1,396,262**

**“Idadi ya wajane Tanzania imefikia 1,396,262, kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.” Waziri Dorothy Gwajima**

**Na Romana Mallya**

SHERIA ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2009 inamtambua mtoto hadi umri wa miaka 18, lakini licha ya kuwapo kwa sheria hii, mtoto mwenye umri wa miaka 11 ameozwa, baada ya miaka mitano, akiwa mjane.

Ni binti wa jamii ya Kimang’ati (jina tunahifadhi) ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 17. Alifiwa na mumewe mwaka 2022, mwaka uliofuata akajiunga Chama cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT) akiwa tayari na watoto wawili wa mwisho mwenye miaka mitatu.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi, Katibu wa chama hicho, Sabrina Tenganamba, anasimulia kisa hicho, akisema kuwa mwanachama wao huyo ndiye mwenye umri mdogo. Mwanachama mwenye mkubwa kuliko wote ni mwenye miaka 90.

Akisimulia safari yake, Sabrina anasema kuwa mwaka 2023 walimpokea binti huyo kuwa mwanachama wao baada ya kuwatafuta kutokana na changamoto zilizokuwa zinamkabili.

“Anatoka jamii ya wafugaji sehemu moja inaitwa Forest, Mkoa wa Pwani, ana watoto wawili. Kesi yake ilikuwa baada ya kufiwa na mume wake kulingana na tamaduni zao, akarithiwa.

“Maisha yake baada ya kurithiwa yakabadilika, akawa si mama wa kulea watoto tena, muda mwingi ulikuwa ni kushinda na mifugo porini. Katika maelezo yake alituambia nilijiona kama mtumwa kule porini. Nimewatafuta kuwaomba mnisaidie’.

“Kama nilivyokueleza mwandishi, chama chetu kipo mikoa mbalimbali, huwa tunatembelea maeneo tofauti. Alitueleza hana nyumba wala pa kukaa kwa sababu kule kwao ni porini, wanamiliki ng’ombe tu. Na kwa mujibu wa tamaduni zao, yeye kama mwanamke wa wafugaji si mmiliki wa hiyo mifugo, hana fursa binafsi ya kumiliki ng’ombe.

“Alitusimulia changamoto zake nyingi ikiwa ni pamoja na kukosa fursa ya kwenda shuleni. Tukamwuliza kwa wakati huo anataka nini? Tulijua angetuambia ujasiriamali kutokana na jukumu la malezi alilonalo, lakini yeye akawa tofauti, akasema anataka kusoma,” anasimulia katibu huyo.

Sabrina anasema wanachama wao wengi wanapowapokea huangukia katika ujasiriamali, lakini kwa mjane huyo ilikuwa tofauti.

“Yeye akawa tofauti, akatuambia anataka kusoma, yaani kuanza elimu ya msingi. Kwa kuwa, mimi nina ofisi Bagamoyo na ni mchungaji, hivyo chama kikaamua kumpeleka shule na watoto wake nikawachukua ili mama yao apate muda wa kutosha wa kujisomea kutimiza ndoto yake ya kupata elimu,” anasema.

Sabrina anabainisha kuwa binti huyo kwa sasa anaishi makao ya nyumba salama huko Pwani na anasoma kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Wanaokosa (MEMKWA) na kutokana na maendeleo mazuri darasani, amevushwa hadi darasa la sita.

Sabrina anafafanua kuwa chama chao, pamoja na mambo mengine, hulenga kusaidia wanawake wajane kutimiza ndoto zao kulingana na hali zao, lengo ni kujikwamua kiuchumi na kutunza familia walizoachiwa.

**KILIO CHAO**

Sabrina anaomba serikali kupitia taasisi zake za fedha pamoja na sekta binafsi zinazotoa mikopo yenye riba nafuu, wasaidie wajane wanaofanya biashara ndogo kwa kupunguza riba za mikopo ili wanufaike na kukuza biashara.

“Hizi riba za kausha damu tutapoteza wajane wengi na tutapoteza taifa kwa ujumla ambalo ni kundi la watoto wanaoachwa baada ya baba zao kufariki dunia. Wanajikuta katika malezi ya upande mmoja, tena kwa mwanamke asiye na kipato na mwingine akiwa hana mali,” anasema.

Katibu huyo anasema chama chao kina mwanasaikolojia ambaye huwasaidia wajane ambao huingia ndani ya chama wakiwa hawana mwelekeo wa maisha huku wakiwa wamekata tamaa kutokana na madhila waliyokutana nayo baada ya kufiwa na kuhitaji ushauri kutoka kwa msaikolojia.

“Msaikolojia hukaa nao mpaka wakae vizuri na wanapoonesha kupona yale yanayowanasibu ndipo chama kinachukua jukumu lake la kuwasaidia kufikia malengo yao.

“Wengine tunawaunganisha na wafanyabiashara wadogo, mfano wanaotengeneza batiki, wanajifunza na baadaye wanakuwa wajasiriamali,” anasema.

**MSAIKOLOJIA ALONGA**

Lucas Sanga, msaikolojia tiba, anayetoa msaada wa kisaikolojia kwa wajane katika chama hicho anataja changamoto kubwa anazokutana nazo mara kwa mara na namna anavyozitatua.

Sanga anasema wengi anaokutana nao huwa wamekata tamaa kwa kuwa walikuwa wanategemea waume zao kwa asilimia kubwa na hawakuweka utaratibu wa kusimama wenyewe.

“Wapo ambao hufikiri ujane ni ulemavu na wanatamani kuonewa huruma. Wengi wanaofika kwangu wanakuwa wameingia katika migogoro ya kifamilia na ndugu upande wa mume, baadhi wanakuwa wamekata tamaa kwa kuhofia kurogwa na kuogopa kupigania haki zao,” anasema.

Sanga anasema kwa wajane wenye umri mkubwa baadhi hufika kwake wakiwa katika hali ngumu kiafya kutokana na kushambuliwa na magonjwa kama presha, sukari, saratani na baadhi huwa na hofu ya kwenda hospitalini kupima baada ya waume zao kufariki dunia kutokana na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI).

“Wanakuja kwangu wakiwa na hofu ya kwenda kupima ili kujua hali za afya zao. Wanapokuja huwa ninawasaidia kwa kuwapa ushauri na mwishowe kuchukua hatua ya kwenda hospitalini,” anasema.

Msaikolojia Sanga anasimulia moja ya visa alivyokutana navyo ni mjane ambaye watoto wake pamoja na ndugu wa mume wake waliungana na kumtuhumu kuhusika na kifo cha mumewe na hivyo kufikia hatua ya kumnyang’anya baadhi ya mali.

“Bahati nzuri hawakuchukua nyumba. Alikuwa amekata tamaa, lakini nilimsaidia na sasa anajishughulisha na ufugaji wa kuku. Tulimpatia kuku 50 kama mtaji wake na kwa sasa anaendelea vizuri,” anasema.

**HATUA SERIKALINI**

Novemba 12, 2022, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akizindua Chama cha Wanawake Wajane Tanzania Tawi la Mkoa wa Dar es Salaam, alisema kwa mwaka 2020, Ofisi ya Takwimu Tanzania ilikadiria kuwapo wajane 880,000 ambao ni sawa na asilimia 3.1 ya wanawake wote ambao mwaka huo walikadiriwa kuwa ni milioni 28.5.

Katika maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani mwaka 2023, Waziri Gwajima alisema idadi ya wajane Tanzania imefikia 1,396,262, kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Alisema takwimu za duniani zinaonesha kuwapo wajane takribani milioni 258 na kati yao, wajane milioni 115 wanadhulumiwa, wanafanyiwa ukatili, wanakabiliwa na umaskini na kutengwa na jamii.

Waziri Gwajima alisema kuwa mbali na kutambua Siku ya Wajane Duniani, Serikali ya Tanzania pia imeweka mifumo ya kulinda haki zao na kuongeza huduma za msaada wa kisheria kwa kutungwa Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya Mwaka 2017.

Alisema kuwa mwaka 2021, serikali ilitoa msaada wa kisheria kwa wajane ambapo kesi 277 za miradhi zilitolewa hukumu ya ushindi ikiwa ni pamoja na uendeshaji mashauri na hukumu katika utetezi wa haki.

Pia alisema kumeanzishwa madawati ya jinsia na watoto 420 katika vituo vya Jeshi la Polisi na vituo 153 katika Jeshi la Magereza kwa lengo la kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa waathirika, wakiwamo wajane.

Kampeni ya Maadili Yetu Taifa Letu - Kuwatunza na Kuwalinda Wajane ni Moja ya Maadili Yetu’ aliitaja ni sehemu ya mikakati ya kutoa elimu kwa jamii kuachana na ukatili wa kijinsia kwa kushirikisha wanaume.

Vilevile, Waziri Gwajima alisema wizara inaendelea kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) ambao katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 664.5 ilitolewa kwa wanawake wajasiamali 104, wakiwamo wajane.

Pia alisema Sheria ya Ardhi ya Kijiji Na. 5 ya Mwaka 1999, Kifungu cha 20(1), inatoa nafasi kwa wanawake, wakiwamo wajane kumiliki ardhi.

Alisema serikali pia inatekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18-2021/22), wakiwamo wajane.

Siku ya Wajane Duniani huadhimishwa Juni 23 kila mwaka. Siku hii ilianzisiwa na Lord Loomba, mwanzilishi wa Loomba Foundation mwaka 2005 baada ya baba yake kufariki dunia Juni 23, 1954.

Umoja wa Mataifa ulipitisha siku hiyo kuwa ya kimataifa kupitia Azimio Na. A/RES/65/189 la Desemba 21, 2010 ambayo hutoa fursa kwa wajane na wadau kutafakari mipango, mikakati, mafanikio na changamoto wanazokumbana nazo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika kuzitatua.

HABARI KITAIFA

# NMB yaipiga jeki serikali hoja ya CAG sekta elimu

**Na Mwandishi Wetu,** NYASA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Machi 2017 alitoa ripoti ya ukaguzi maalum wa miundombinu na samani za shule za msingi nchini, ambapo anaitaka serikali kujenga shule mpya na kufanya ukarabati kwa shule zinazokabiliwa na uchakavu.

Katika kuunga mkono serikali kutekeleza hoja hiyo ya CAG, Benki ya NMB imetoa msaada wa vifaa mbalimbali vya ujenzi vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 29.7 kwa shule sita zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma.

Akizungumza kwenye hafla ya ugawaji wa vifaa hivyo iliyofanyika katika Shule ya Msingi Nangombo, mjini Mbambabay juzi, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Faraja Ng'ingo alitaja vifaa vilivyotolewa na benki hiyo kuwa ni mabati na misumari kwa ajili ya kuezekea.

Alitaja shule zilizonufaika na msaada huo ni tano za msingi ambazo ni: Nangombo iliyopata vifaa vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni tano; Chiwindi iliyopatiwa vifaa vya Sh. milioni 4.6; Lundo iliyopata vifaa vya Sh. milioni 4.5; Chinula iliyopewa vifaa vya Sh. milioni 4.28; Ndingine iliyopata vifaa vya Sh. milioni 6.9 na Shule ya Sekondari Ngumbo ambayo imepewa vifaa vya Sh. milioni 4.28.

"Vifaa hivi tunavyokabidhi leo (juzi) ni moja ya ushiriki wetu katika maendeleo ya jamii, sisi kama benki tunao wajibu wa kuhakikisha jamii inayotuzunguka inafaidika kutokana na faida tunayoipata," alisisitiza Ngingo.

Alisema kwa miaka kadhaa, NMB imekuwa inasaidia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi kwa kujikita zaidi kwenye miradi ya elimu kwa kutoa madawati na vifaa vya kuezekea na sekta ya afya kwa kutoa magodoro, vitanda na vifaa vingine vya kusaidia matibabu.

Mgeni rasmi kwenye hafla hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyasa, Salum Ismail alishukuru Benki ya NMB kwa msaada wa vifaa hivyo, akisema benki hiyo imekuwa inatoa misaada mbalimbali serikalini katika sekta za elimu na afya.

Alisema benki hiyo pia imekuwa inatoa mchango mkubwa kwenye majanga ambapo katika Wilaya ya Nyasa, NMB imeshiriki kutoa vifaa "vya huruma" yakiwamo majeneza kwa watu tisa waliopoteza maisha hivi karibuni kwa ajali ya gari katika Kata ya Lumeme.

Alitoa rai kwa walimu wa shule ambazo zimekabidhiwa vifaa hivyo vya kuezekea kuhakikisha vinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa, pia wazazi na walezi kuendelea kusimamia maadili na nidhamu ya watoto wao tangu wakiwa nyumbani.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Pasifiki Mhapa alisema NMB imekuwa karibu sana na jamii katika kuhakikisha changamoto za elimu na afya zinapatiwa ufumbuzi.

Hata hivyo, Mhapa alisema mahitaji ya kielimu katika halmashauri hiyo bado ni makubwa kutokana na idadi ya watoto kuongezeka, hivyo halmashauri inahitaji wadau kama NMB kusaidia katika maendeleo yaa elimu.

Akizungumza kwa niaba ya walimu wa wakuu waliopata msaada wa vifaa hivyo, Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Chinula Mwl. Emanuel Chilwa aliishukuru NMB kwa msaada huo ambao unakwenda kupunguza changamoto ya vifaa vya ujenzi katika shule hizo.

NMB ni benki yenye matawi zaidi ya 231 nchini, ikiwa na mashine za kutolea fedha (ATM) zaidi ya 715 nchi nzima, mawakala zaidi ya 30,000 na wateja zaidi ya milioni sita.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2021/22 iliyowasilishwa bungeni Aprili 6, 2023, CAG Charles Kichere anaeleza kuwa tathmini yake kuhusu miundombinu ya shule za msingi za halmashauri 45 alizozikagua, ilibaini zilikuwa na upungufu wa madarasa 27,316, madawati 158,066, vyoo 56,530 kwa ajili ya wanafunzi na nyumba za walimu 35,684.

Jedwali la uhaba wa miundombinu ya shule za msingi.

| Miundombinu | Mahitaji | Yaliyopo | Upungufu |
|---|---|---|---|
| **Madawati** | 596,872 | 438,806 | 158,066 |
| **Vyoo (funzi)** | 100,630 | 44,100 | 56,530 |
| **Nyumba (wal)** | 45,557 | 9,873 | 35,684 |
| **Viti na meza** | 63,764 | 33,935 | 29,829 |
| **Madarasa** | 57,866 | 30,550 | 27,316 |
| **Ofisi walimu** | 4,997 | 2,731 | 2,266 |
| **Vyoo walimu** | 1,520 | 898 | 622 |
| **JUMLA** | **871,206** | **560,893** | **310,313** |

CHANZO: Ripoti ya CAG, Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa 2021/22 (Uk. 116).



Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa pamoja wa wadau wa Usafiri wa Anga nchini kujadili kwa pamoja mustakabali wa namna ambavyo Tanzania itajiunga katika Soko la Pamoja la Usafiri wa Anga Afrika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# V8 lenye bendera ya chama lanaswa likisafirisha wahamiaji haramu 20

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

JESHI la Polisi mkoani Manyara linamshikilia mkazi wa Dodoma, Edward Erihard (31) kwa kosa la kuwasafirisha wahamiaji haramu 20 raia wa Ethiopia kinyume cha sheria.

Taarifa ya kukamatwa kwa wahamiaji hao haramu ilitolewa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Kamishna Msaidizi Lucas Mwakatundu.

Kamanda Mwakatundu alisema wahamiaji hao walikamatwa Machi 23, mwaka huu katika kizuizi cha magari cha Minjingu kilichoko wilayani Babati, barabara kuu ya Arusha-Babati.

Alisema Erihard alikamatwa akiwa anawasafirisha wahamiaji hao 20 kwa kutumia gari lenye namba za usajili T 774 BDL Land Cruiser, lililokuwa na bendera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aliwataja waliokamatwa ni Samweli Achiso (23), Breano Asata (25) na wenzao 18 ambapo taratibu nyingine za kisheria zikikamilishwa, watafikishwa mahakamani.

Vilevile, alionya watanzania wasio wazalendo wanaojihusisha na uhalifu, hususani usafirishaji wahamiaji haramu, akiwataka kuacha mara moja kwa kuwa ni hatari kwa usalama wao.

Mkazi wa Mtaa wa Negamsi, Daniel Sanka alidai kutumia bendera ya CCM ni mbinu ya uhalifu ili kujilinda asikamatwe.

Mkazi wa Magugu, Paul John alidai mbinu hiyo ya kutumia bendera ya CCM inatoa ishara ya kuwapo mtandao wa viongozi ndani ya chama anashirikiana nao ili kufanya uhalifu huo.

John alisema si jambo la kawaida mtu kuwa na ujasiri wa kuweka bendera ya chama tawala kwenye gari lililobeba wahamiaji haramu. Alisisitiza uchunguzi wa kina ufanyike ili kubaini mtandao wa biashara hiyo haramu.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maelekezo ya Rais Samia yanasubiriwa kwa hamu hatima uchumi vyombo vya habari

**JUZI** wakati Msemaji Mkuu wa Serikali akiongea na Wahariri na Waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari nchini, kuhusu miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, alizungumzia hatua iliyofikia kamati iliyoundwa kwa ajili ya kutathmini hali ya utendaji na uchumi kwenye vyombo vya habari.

Taarifa njema ni kwamba kamati hiyo imeshamaliza kazi yake na ripoti yake inatarajiwa kukabidhiwa hivi karibuni kwa Rais Samia.

Vyombo vya habari kwa sasa vinapitia wakati mgumu kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya habari baada ya biashara nyingi kuhamia kwenye mitandao.

Biashara kubwa iliyokuwa inategemewa ya uzalishaji wa magazeti imeporomoka kutokana na watu wengi kupata habari kupitia kwenye simu zao na mitandao ya kijamii.

Hata nchi zilizoendelea ambazo zilikuwa zinaongoza kwa kuuza magazeti mengi sasa zimebadili mfumo na kwenda kimtandao kwa kupunguza idadi ya uchapishaji magazeti.

Hali hiyo imeathiri uchumi wa vyombo vya habari ambavyo vilikuwa vikitegemea matangazo yanayouzwa kwenye magazeti yao kujiendesha.

Hivi sasa sekta ya habari imevamiwa kila mtu mwenye simu ya mkononi anaweza akarekodi tukio na kusambaza kupitia mitandao ya kijamii na wakati mwingine habari hiyo inakosa maadili, lakini imeshasambaa.

Wakati mwingine hata watangazaji wanaamua kupeleka matangazo yao kwa watu hao wanaoanzisha mitandao ya kijamii ambayo inatembelewa na watu wengi, wakiamini kuwa matangazo yao yatasomeka zaidi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Nape Nnauye, aliteua kamati ya kutathimini hali ya utendaji na uchumi kwenye vyombo vya habari na kuelekeza kuwa dhamira ni serikali ni kushughulikia suala la uchumi kwa vyombo vya habari.

Vyombo vya habari hasa vya binafsi havipati ruzuku yoyote ya kujiendesha, inategemea matangazo kutoka kwa watangazaji wao.

Hata hivyo, upatikanaji wa matangazo hayo umekuwa mgumu na hata wanaotangaza ulipaji wao sio wa kuridhisha kutokana na wengine kukaa na deni hata zaidi ya mwaka, hali inayokwamisha vyombo vingi vya habari kufanya kazi yao kwa ufanisi.

Baadhi ya vyombo vya habari vinashindwa kulipa wafanyakazi wake kwa wakati kwasababu ya kudai madeni ya muda mrefu kutoka kwa watangazaji wake.

Pia, kuna gharama za uendeshaji. Kwa mfano kwa vyombo vya magazeti kuna gharama ya kuagiza karatasi za kuchapishia pamoja na ushuru.


Kinachotia moyo ni kusikia habari njema kuwa ripoti hiyo karibu itatua mikononi mwa Rais na Rais Samia toka alivyoingia madarakani amekuwa karibu sana na vyombo vya habari kwa kukutana na viongozi wa vyombo hivyo na kujadiliana hali halisi inayowakabili.

Kilio kikubwa cha vyombo vya habari ni kulipwa madeni yao ambayo wanazidai taasisi mbalimbali zikiwamo za serikali kwa muda mrefu.

Kilio hichi pia kiliwasilishwa kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kuagiza taasisi zote zinazodaiwa zilipe madeni hayo, lakini vyombo vingi vinalalamika kutolipwa.

Ndio maana tunasema maagizo ya Rais Samia baada ya kukabidhiwa ripoti hiyo yanasubiriwa kwa hamu kujua hatima ya vyombo vya habari ambavyo vinapitia hali ngumu ya kiuchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

Na Flavian Jeremiah

# Mabadiliko ya tabianchi yanavyoweza kuathiri Dira ya Maendeleo Taifa ijayo

**TUNAKUMBUKA** serikali nchini ilitengeneza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, katika kuongoza harakati ya maendeleo ya uchumi na jamii kwa taifa.

Hiyo hata ikawa msaada, kuiwezesha nchi kufikia hadhi ya nchi zenye kipato cha kati na kuondokana na idadi kubwa ya umasikini uliokithiri kwa Watanzania.

Uboreshaji wa hali ya maisha ya Watanzania, ni kujenga utawala bora na kuhakikisha kunakuwapo mazingira ya amani, usalama na umoja, kutengeneza jamii iliyoelimika vyema, kukijenga uchumi imara nchini.

Ni vitu vilivyopewa kipaumbele katika Dira Maendeleo ya Taifa. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na taasisi na mashirika binafsi ya ndani na nje ya nchi, kumekuwapo athari kubwa zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi katika uchumi kama.

Hapo unaingia mfano wa sekta ya kilimo kinachotegemewa na idadi kubwa ya Watanzania, wastani asilimia 75 na mifumo ya biashara ya kimataifa. Hata hivyo, kama nchi tunakwazwa kufikia baadhi ya malengo katika mikakati ya Dira ya Maendeleo 2025.

Inaangukiwa na sababu kama, milipuko wa janga la maradhi Uviko 19, athari za mabadiliko ya tabianchi, ambazo zimekuwa tishio kubwa kwa uchumi wa taifa

Mabadiliko hayo ya tabianchi, yameleta athari kubwa katika sekta kubwa na muhimu zinazotegemewa na serikali, pamoja na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Hivyo zimekuwa miongoni mwa vikwazo vinavyokwamisha maendeleo, pamoja na jitihada zinzochukuliwa kupunguza athari tajwa za mabadiliko ya tabianchi.

Sasa, katika kuelekea Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, kama nchi pamoja tuna wajibu wa kuhakikisha tunaongeza nguvu katika kupambana na janga hilo, ili kupunguza athari tajwa, kwani kufikia mwaka 2050 inakadiriwa sekta za kilimo, uvuvi pamoja ma ufugaji zitaathiriwa zaidi, hata kupunguza shughuli hizo kwa asilimia 2.8.

Ni athari zinazochangia katika upatikanaji ajira, pia chakula cha kutosha, viwanda na biashara navyo havibaki salama.

Kuguswa huko kwa sekta muhimu, kinamana katika uwanda wa pato la taifa, matarajio ni kupungua kwa chini ya asilimia moja katika safari kusonga mwaka 2030 kuchumi. Hivyo ni jambo linalotujengea wajibu wa kila

mmoja kuendelea kupambana kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwani huathri kila mtu.

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, tunajua iko mahali hapo kushirikiana na taasisi na mashirika ya ndani na kimataifa zikichukua tahadhari na kuunda mikakati, pia sera wezeshi zinazopunguza vyanzo vya mabadiliko ya tabia nchi na kujenga uwezo wa kuendelea kukabiliana na athari zake.

Hizo ni pamoja na kuendelea na matumizi ya nishati safi na ufanisi kama vile umeme na gesi asilia, matumizi ya mkaa mbadala na vyanzo vinginevyo ambavyo ni nafuu kwa watu, vikiendana na uhalisia wa uchumi wa Watanzania, ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kama vyanzo vya msingi vya nishati.

Ipo nafasi inayotajwa ya kuendelea kujenga miundombinu inayo weza kuimiri athari ya mabadiliko ya tabianchi, hasa mvua ambazo zimekuwa zikichangia mafuriko na uharibifu wa miundombinu, hata kuwajibisha serikali kujenga madaraja imara.

Jitihada nyinginezo ni za kutolewa elimu ya kutosha kwa watu juu ya mabadiliko ya tabianchi, teknolojia za kupunguza vyanzo vya uchafuzi mazingira (vinavyosababisha kutokea kwa mabadiliko ya tabianchi), kusimamia sheria na sera za mazingira.

Dhamira hapo inatajwa kuwa ni kuhakiksha hatua za utunzaji mazingira kupunguza mabadiliko ya tabianchi zinazingatiwa katika kila sekta za uchumi, kuliwezesha taifa kufikia malengo yatakayopangwa katika Dira ya Taifa ya 2025-2050.

# ‘Kuna maofisa TAMISEMI wanakingia kifua walaji wa fedha za halmashauri’

**Na Steven William,** MUHEZA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imesema baadhi ya maofisi katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wanalinda wabadhirifu wa fedha kwenye halmashauri kwa kuwakumbatia ili wasichukuliwa hatua.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Halima Mdee alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika majumuisho ya ziara yao baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Chatuu na Hospitali ya Wilaya ya Muheza.

Mdee, akizungumza kwa ukali, alisema kumekuwa na tabia Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuwakingia kifua watumishi ambao wamefanya ubadhirifu wa fedha za serikali huku kutokana na alichokitaja kuwa urafiki, undugu au kushirikiana kufanya ubadhirifu .

Alionya kuwa kamati hiyo chini ya uongozi wake halikubaliani na hilo; kiongozi yeyote atakayekula fedha za serikali, ajue atafikishwa mahakamani akibainika.

Mdee alisema LAAC inaelekeza Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufuatilia na kufanya uchunguzi wa fedha walizopeleka kutekeleza miradi katika maeneo mbalimbali kama zimetumika kwa lengo lililokusudiwa.

Alisema miradi ya maendeleo ipo kwa manufaa ya wananchi, hivyo kamati yake inaagiza kuwe na ufuatiliaji wa fedha za miradi hiyo na usimamizi wake.

Mdee pia aliwanyooshea kidole viongozi wa Mkoa wa Tanga kwa kushindwa kufuatilia na kusimamia miradi ya maendeleo katika wilaya za mkoa huo.

“Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa inaelekeza Ofisi ya Rais – TAMISEMI na CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) kufanya ufuatiliaji na uchunguzi wa fedha walizopeleka kutekeleza miradi katika maeneo mbalimbali kama zimetumika kwa usahihi,” aliagiza Mdee.

Alisema ikibainika fedha za serikali zimepelekwa sehemu husika kisha kumefanyika ubadhirifu, wahusika wakamatwe na kushtakiwa kwa kuhujumu uchumi; hata kama wamehama watafutwe wakamatwe.

Mdee alisema, “Kumekuwa na tabia Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuwakingia kifua watumishi ambao wamefanya ubadhirifu wa fedha za serikali kutokana na urafiki, undugu au kushirikiana kufanya ubadhirifu,” alionya.

Mjumbe wa kamati hiyo, Ester Bulaya alisema kuwa katika halmashauri nyingi, miradi haina ubora na serikali imepeleka fedha za kutosha.

Kukabiliana na hilo, mjumbe huyo alisema ni lazima watumishi walioteuliwa na Rais wamsaidie kwa kujitafakari wemepewa nafasi hiyo wafanye mazuri, waache alama ili hata wakiondoka wabaki wanakumbukwa.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainabu Abdallah alisema maagizo yote yaliyotolewa na kamati hiyo kuhusu Wilaya ya Muheza yatafanyiwa kazi kwa kusimamia miradi ikamilike kwa wakati na ubora zaidi pamoja na kusimamia matumizi ya fedha za miradi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina alisema maagizo yote ameyasikia kutoka kwa kamati hiyo ya Bunge, watayafanyia kazi na miradi itakamilika kwa wakati na ubora katika halmashauri hiyo na watasimamia matumizi sahihi ya fedha za serikali.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Erasto Mhina alishukuru serikali kwa kupeleka fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo, akiahidi kusimamia miradi hiyo ili iwe na ubora na kukamilika kwa wakati.

Wajumbe wa LAAC wanaendelea na ziara kwenye wilaya zingine za Korogwe, Pangani, Tanga na Mkinga, mkoani Tanga.

# Kumekucha ripoti ya CAG ikitua kwa Rais juma hili

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO wa Bunge la Bajeti umepangwa kufanyika kuanzia Jumanne ya juma lijalo. Pamoja na mambo mengine, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 itawasilishwa kwa mujibu wa sheria.

Ibara ya 143 ya Katiba ya nchi (1977), inaelekeza CAG kuwasilisha kwa Rais taarifa yake ya ukaguzi.

Katiba hiyo inaelekeza pia kitika kifungu hicho kuwa, baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho.

Kwa kuzingatia, Ijumaa itakuwa sikukuu, ripoti ya CAG itawasilishwa kwa Rais kati ya leo na Alhamisi ya juma hili ili kukidhi maelekezo ya kikatiba.

CAG amekuwa akiandaa ripoti za ukaguzi wa mwaka zikijumuisha Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu; Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa; Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Ukaguzi wa Ufanisi. Pia amekuwa akiandaa ripoti za Ukaguzi Maalum.

Ripoti ya mwaka 2022/23, kama ilivyokuwa katika ripoti zilizopita, inatarajiwa kugusia ukusanyaji wa kodi kutoka vyanzo mbalimbali, uandaaji na utekelezaji bajeti ya serikali, hali ya Deni la Serikali, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa mali na madeni ya serikali pamoja na usimamizi na uendeshaji wa taasisi za umma.

Baada ya kuwasilishwa bungeni na mawaziri husika, Ripoti ya CAG itakabidhiwa kwa kamati za Bunge zenye mamlaka ya kuifanyia uchambuzi. Miongoni mwa yanayotarajiwa kuwa gumzo katika ripoti ya CAG ni madai ya kuwapo ufujaji wa fedha za umma unaodaiwa kufanywa na maofisa wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wakishirikiana na watendaji wa serikali, pia upigaji wa fedha miradi inayosimamiwa na taasisi na mashirika ya umma na ‘mchwa’ wa fedha za maendeleo katika halmashauri mbalimbali hasa mikoa yenye miradi mikubwa.

Hoja nyingine ni kukua kwa kasi kwa Deni la Serikali na utendaji usioridhisha wa kujiendesha kwa hasara ya mabilioni, hali ya miundombinu ya sekta za elimu na maji, pia majibu ya serikali kuhusu hoja zilizopita, zikiwamo malipo ya mamilioni ya shilingi kutunza vyura Marekani na hujuma katika ghala la pembe za ndovu jijini Dar es Salaam.

Vilevile, Ripoti ya CAG inatarajiwa kuangazia hali ya mifuko ya hifadhi ya jamii na uwiano wa kazi na watumishi waliopo, hasa katika sekta za elimu na afya.


OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI
(IDA CREDIT NO. 7215-TZ)

## TANGAZO KWA UMMA

**ZOEZI LA UBOMOAJI WA NYUMBA ZILIZOFIDIWA NA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) alianza kuwalipa fidia waathirika wa mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kuanzia mwezi Novemba 2023. Kwa mujibu wa makubaliano ya ulipaji wa fidia, waathirika wanatakiwa kupisha eneo la mradi ndani ya wiki sita (6) baada kupokea fedha kwenye akaunti zao. Muda huu umeshakamilika kwa idadi kubwa ya waathirika.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa kushirikiana na ofisi za Wakurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni, inatarajia kuendesha zoezi la ubomoaji wa nyumba zilizofidiwa kuanzia tarehe 12/04/2024. Hivyo waathirika wa mradi wanatakiwa kupisha eneo la mradi kabla ya tarehe tajwa hapo juu. Ikumbukwe kuwa ubomoaji huu unawahusu waathirika wa mradi ambao wameshapokea fidia katika akaunti zao kwa muda usiopungua wiki sita (6) tangu siku ya kuanza zoezi hili.

KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

# EPZA yahimiza halmashauri kutenga maeneo ya uwekezaji wa viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA) imezihimiza halmashauri za wilaya kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye viwanda.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe akiwa katika ziara ya ufuatiliaji na tathmini ya wawekezaji wenye leseni za Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZ) na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya SEZ katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Tabora na Singida.

"Kuwapo maeneo maalum ya EPZ na SEZ yakiwa na miundombinu ya msingi ni mojawapo ya vitu muhimu ambavyo huwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye viwanda nchini," alisema.

Itembe alibainisha hayo kwa nyakati tofauti wakati akizungumza na Makatibu Tawala Wasaidizi - Uwekezaji, Viwanda na Biashara wa mikoa ya Mwanza, Geita na Tabora.

Alisema kuwa halmashauri husika zitapata mapato yatokanayo na kukodisha maeneo hayo kwa wawekezaji pamoja na faida pana ya kuongeza ajira, kuvutia mitaji, kuongeza mauzo ya nje, kufungamanisha uzalishaji malighafi za kilimo, madini, uvuvi na misitu pamoja na uchakataji viwandani, hivyo kuongeza thamani bidhaa hizo.

Alihimiza mikoa ya Mwanza, Geita na Tabora ambayo hadi sasa ina mwekezaji mmoja mmoja tu, idadi ambayo ni ndogo sana, kushirikiana na Mamlaka ya EPZ kujenga mazingira wezeshi ya kuvutia na kuhamasisha wawekezaji wengi kutoka ndani na nje ya nchi.

Itembe alipongeza juhudi na hatua zinazofanywa na Halmashauri ya Mji wa Geita, Manispaa ya Ilemela na Halmashauri ya Mji wa Kahama kwa kutenga maeneo ya uwekezaji na kuandaa mpango kabambe wa uendelezaji maeneo hayo.

Aliwataka viongozi wa halmashauri na manispaa nyingine nchini kote kuiga mfano wa Geita, Ilemela na Kahama ili kuweza kunufaika na uwekezaji wa viwanda kupitia Mamlaka ya EPZ.

Sambamba na zoezi hilo la ufuatiliaji na tathmini ya wawekezaji wenye leseni za EPZA, pia alipata fursa ya kutembelea ofisi za mikoa na halmashauri kwa lengo la kueneza uelewa wa majukumu na malengo ya kisera ya Mamlaka ya EPZ, na kuhamasisha serikali za mitaa na tawala za mikoa kushiriki katika uwekezaji wa kanda maalum za kiuchumi kwa kushirikiana na EPZA ili kunufaika na fursa zipatikanazo.

Katika kukamilisha ziara hiyo, ilikubalika kuwa uongozi wa mkoa kushirikishana ratiba ya vikao vya kamati za ushauri wa mikoa ili wataalamu wa Mamlaka ya EPZ kuja kuwajengea ufahamu wa fursa za uwekezaji kipitia maeneo ya EPZ na SEZ.

"Aidha ofisi za mikoa na halmashauri zake kushirikiana na Mamlaka ya EPZ kutangaza fursa za uwekezaji zilzopo katika mikoa husika," alisisitiza.

Mkurugenzi Mkuu wa Mkuu wa EPZA aliwasihi maofisa wa ngazi ya mkoa na halmashauri kuendelea kuwahudumia wawekezaji walio chini ya EPZA kwa mujibu ya matakwa ya sheria zinazowaongoza, ikiwamo Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2019 ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan.

"Leseni kutoka EPZA huambatana na hadidu za rejea (terms of reference) ambazo wawekezaji wanapaswa kuzifuata, mojawapo ikiwa ni kuwa na Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) na halmashauri alipo mwekezaji huyo. Hivyo, watumie fursa hii pia kuhakikisha wawekezaji wanawajibika kwa jamii," aliagiza.

Katika ziara yake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya EPZ, pia alishiriki uzinduzi wa chuo cha mafunzo kwa wafanyakazi migodini (Buzwagi Academy) kilichozinduliwa katika ukanda wa kiuchumi wa Buzwagi-SEZ ulionzishwa kama hatua za ufungaji wa mradi wa ubia baina ya Manispaa ya Kahama na kampuni ya Twiga.

Aidha, Mamlaka ya EPZA ipo mbioni kusajili kampuni zipatazo nane zilizokwishaonesha nia ya kuwekeza katika ukanda huo wa kiuchumi wa Buzwagi.

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Geita, Charles Chacha alibainisha kuwa kuna taasisi nyingi nchini lakini hazijulikani katika ngazi ya serikali za mitaa na tawala za mikoa, hivyo kushindwa kutumia ipasavyo fursa mbalimbali na pia kupelekea kushindwa kuwahudumia ipasavyo wawekezaji wenye leseni za EPZ na SEZ katika maeneo yao.

Sababu hiyo ilibainishwa pia na Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora Dk. John Mboya, akipendekeza kuandaa programu maalum ya kuonesha fursa hizo kwa viongozi wa mkoa na halmashauri.



Waziri wa nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) Dk.Kitila Mkumbo (kulia) akimpongeza mshindi wa tuzo ya Malkia wa Nguvu ajaye,Jennifer Dickson katika hafla ya kutunuku tuzo hizo iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Katikati ni mwenyekiti wa bodi ya maktaba ya kijamii ya Mwanga iliyoanzishwa na Jennifer, Profesa Bonaventure Rutinwa, ambaye pia ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wafundishwa kilimo bora cha nyanya

**Na Francis Godwin,** IRINGA

VIJANA 140 kutoka familia zenye mazingira magumu katika Kata za Mdabulo, Ihanu na Luhunga wilayani Mufindi, mkoani Iringa wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha zao la nyanya ili walime kwa tija na kuinua uchumi wao.

Akizungumza jana baada ya mafunzo hayo Mufindi, mkufunzi Jerry Chang'a, alisema kuwa ardhi ya Mufindi ni yenye rutuba inayofaa kwa kilimo kuwezesha wengi kuvuna kwa wingi, lakini wakulima wa mahindi na maharage wameendeleza kilimo cha mazoea.

Aidha, alisema anaamini kupitia mafunzo hayo chini ya mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), vijana wana fursa ya kutumia mafunzo kujikita kwenye kilimo bora cha nyanya ambacho kitawakomboa kimaisha.

Alisema kwa sasa wananchi wa Luhunga, Ihanu na Mdabulo wanategemea nyanya kutoka soko la Mafinga umbali wa zaidi ya kilomita 55 na huuzwa moja kwa Sh. 100 ambayo wangeweza kulima kwa wingi na kupata pesa za kutosha.

"Mfano Kata ya Luhunga wananchi tunauziwa nyanya moja Sh. 100 wakati ardhi yetu inakubali kilimo hicho kwanini tusilime na kupeleka mjini kuuza kwa bei nzuri," alisema Chang'a.

Aidha, aliwataka vijana hao kuachana na kilimo cha mazoea badala yake kujikita kwenye kilimo bora cha nyanya kinachoweza kulimwa msimu wote kutokana na hali ya hewa ya Mufindi.

Alisema kilimo cha nyanya kitaalamu kwa ekari moja kinauwezo wa kumpatia mkulima Sh. milioni 30 wakati kilimo cha mahindi ni Shilingi milioni saba kwa ekari.

Pia, alisema sehemu kubwa ya vijana hao wana fursa ya ardhi kutokana na ukubwa wa ardhi ya familia zao na kukodi haizidi Sh. 50,000.

Washiriki wa mafunzo hayo, Ferdinando Gandye na Yosepha Mgonidugulu, walisema kabla ya mafunzo hayo walikuwa hawajaona fursa ya kilimo cha nyanya, mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza wigo wa fursa.

Meneja Msaidizi wa Mradi wa YAM, Daniford Mkumba, alisema mafunzo hayo yamehusisha vijana 140 kutoka vijiji 16 vya kata tatu za Wilaya ya Mufindi.

## Amchoma mtoto mikono, miguu madai kuiba 16,000/-

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

MKAZI wa Kata ya Mabatini, Lucia Majura anadaiwa kumchoma mikono na miguu mtoto wa jirani yake akimtuhumu kumwibia Sh. 16,000.

Mtoto huyo mwenye umri wa miaka 11 (jina limehifadhiwa), mkazi wa Majengo, anadaiwa kuunguzwa kwa maji ya moto mikononi na miguuni na jirani huyo akimtuhumu kwa wizi wa Sh.16,000 aliyokuwa amehifadhi ndani kwake.

Lucia anadaiwa kutekeleza ukatili huo Machi 15, mwaka huu baada ya mtoto huyo kwenda kucheza nyumbani kwake na baadaye kusikika akilalamika ameibiwa pesa na kuanza kumwadhibu mtoto huyo.

Akisimulia tukio hilo mtoto huyo alisema alikimbizwa na kukamatwa na watoto wenzake waliompeleka kwa mama huyo na alipofika alianza kuadhibiwa kwa kuchapwa viboko na baadaye kuunguzwa na maji ya moto.

"Walinikuta nacheza nje baada ya kutoka nyumbani kwao wakaniambia twende unaitwa na mama ukachapwe viboko umeiba hela ya mama, tulipofika huyo mama akaanza kunipiga kisha akachemsha maji ya moto kwenye bakuli na kunimwagia mikononi.

"Alivyomaliza akachukua kisu na kuanza kunikata ngozi halafu akachukua kijiko akakiweka kwenye moto kisha kunibandika kwenye vidonda alivyoniunguza," alidai.

Baba wa mtoto huyo (jina linahifadhiwa), alisema baada ya tukio hilo alitoa taarifa kwa viongozi wa mtaa ili kupata msaada zaidi wa kisheria na kumpeleka mtoto kwenye matibabu.

Alisema baadaye alitakiwa kwenda polisi na kupata barua ya kuruhusiwa kupata matibabu (PF3).

Alisema mtuhumiwa alikamatwa na kuachwa kwa dhamana huku uchunguzi ukiendelea Kituo cha Polisi Mwanza kwa kupelekwa mahakamani.

"Sasa hivi matibabu ya mtoto nagharamikia mwenyewe na fedha sina wakati mwingine siendi kwenye majukumu yangu kutokana na mtoto kuhitaji msaada wakati wote," alisema.

Mama mzazi wa mtoto huyo aliiambia Nipashe kuwa wakati tukio hilo linatokea alikuwa nyumbani kwake akiendelea na shughuli za nyumbani, lakini kilio cha mtoto kilimshitua na kuamua kufika kwa jirani yake na kumkuta mwanawe ameloa damu.

Shuhuda wa tukio hilo, Dorica Meckzedeck alisema hakushtushwa na kilio cha kijana huyo kwa kuwa mtaa huo una watoto wengi na kulia lilikuwa suala la kawaida, lakini alishangaa alivyoumuona majeraha hakuamini kama angeadhibiwa kiasi hicho bila kujali umri wake.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Mwenyekiti wa mtaa huo, Raphael Mathias alisema baada ya kupewa taarifa hizo alichukua askari wa jeshi la akiba 'mgambo' na kufika eneo la tukio na kuwachukua wazazi wa mtoto pamoja na mtoto kwenda ofisini kuandika ripoti na baadaye kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi Mabatini kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.



## Mfanyabiashara kujenga misikiti sita, madrasa Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

MFANYABIASHARA raia wa Saudi Arabia, Mohammed Ainahdi, anayeendesha miradi ya uchimbaji wa visima virefu vya maji nchini, ameahidi kujenga misikiti mikubwa sita na madrasa, inayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.4

Hadi kufikia sasa mfanyabiashara huyo tayari ameshachimba visima virefu 86 bure vya majisafi na salama katika Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

Miradi hiyo ya hisani inayolenga kurejesha kwa jamii kile alichokichuma, itajengwa katika Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga.

Ainahdi ni mmiliki wa Taasisi ya Kimataifa ya Mo Maji Well Drilling Limited, inayofanya kazi nchini kwa sasa ya uchimbaji wa visima virefu na ujenzi nyumba za ibada.

Alisema lengo la kujenga misikiti hiyo na madrasa ni kuwaokoa watoto wasiingie katika mmomonyoko wa maadili na makundi yasiyofaa na kujikita kusoma dini.

Alisema haipendezi kuachwa watoto wakizurura mitaani, alisema ni lazima wachukuliwe na wapewe elimu ya dini, ili waje kuwa watu wema na kujitambua.

Alisema kuwa pia kwa sasa katika mwezi wa mfungo wa Ramadhani anatoa huduma ya kuwafuturisha futari wananchi katika vijiji vyote bila kujali dini, kabila wala vyama vya siasa.

**Miradi hiyo ya hisani inayolenga kurejesha kwa jamii kile alichokichuma, itajengwa katika Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga.**

# M/kiti CCM anusa ufisadi ujenzi kituo cha afya, atoa maagizo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha, Thomas Ole Sabaya, amenusa harufu ya ufisadi katika Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Bwawani kilichoko Wilaya ya Arumeru.

Hivyo ameagiza kubadilishwa milango yote ya kituo hicho kipya na kuweka milango ya mbao ngumu kama makisio ya ujenzi yanavyoelekeza pamoja na mwongozo wa serikali.

"Natoa miezi mitatu kwa Halmshauri ya Arusha, kubadilisha milango yote. Hatutaki ubabaishaji Arumeru. Milango ya mninga inafahamika. Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa, tulitembelea kituo hicho cha afya na milango iliyowekwa siyo ya mbao ngumu," alisema.

Kabla ya Sabaya kutuhumu ujenzi huo katika kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM, Mkoa wa Arusha, kuliibuka malumbano kati ya Sabaya na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Salekwa Ojung'u, anayepinga maelekezo ya kamati ya siasa ya mkoa huo, iliyoyatoa kutokana na dosari mbalimbali.

"Mkuu wa Wilaya ya Arumeru (Emmanuela Kaganda), ninakuagiza ukaguzi ufanyike wa kina na maagizo yaliyoazimiwa na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa yatekelezwe ndani ya muda.

Haiwezekani wajumbe tumekwenda na tumejiridhisha kuwa milango siyo ya mbao ngumu, halafu mwenyekiti unakuja hapa unaanza kubishana na wajumbe sitaki ubabaishaji."

Vilevile, Sabaya, alimpa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, mwezi mmoja kumaliza mgogoro wa mapigano ya mara kwa mara, yanayotokea kati ya Kijiji cha Naani na Kisangiro, Wilaya ya Ngorongoro na wakati mwingine kusababisha vifo.

"RC (Mkuu wa Mkoa), nakupa mwezi mmoja huu mgogoro uishe kwa sababu unasababishwa na watu wako ambao ni watumishi wa umma, wanaolima kwenye bonde lilipo kwenye moja ya hivi vijiji, pamoja na madiwani halafu wanawarubuni wananchi, ili wapigane na wao waendelee na kilimo,"alisema.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella aliunga mkono maelekezo hayo ya mwenyekiti na kuongeza kuwa mbao ngumu kwa mujibu wa kanuni za serikali, ni mninga na mkoko, lakini milango iliyopo kwenye kituo hicho cha afya imepigwa rangi.

"Mbao ngumu zinazotumika kwa mujibu wa kanuni ni mkoko na mninga, na huwa hazipakwi rangi zinapakwa clear polish (kemikali ya rangi ya kunakshi mbao). Kwa nini nyie Halmashauri ya Arusha, mmepaka rangi kweli ni mbao ngumu na miradi yenu mingine tuliyotembelea, tumeona milango ya mbao ngumu ikiwa haijapakwa rangi.

Hizi ni mali zetu zitatuhudumia sisi, wajukuu zetu na vizazi vyetu. Sioni sababu ya kufanya udanganyifu tunamdanganya nani na ili iweje ndugu zangu."



Mratibu wa Shirika la Ujamaa Community Resource Team (UCRT) Edward Loure, akizungumza mji mdogo wa Orkesumet kwenye uzinduzi wa mradi wa uhifadhi jumuishi wa mazingira na kuboresha maisha ya jamii kwa Wilaya za Simanjiro na Kiteto mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Sekondari Usagara yaibuka kidedea shindano la AQRB

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), imemkabidhi Mkuu wa Shule ya Sekondari Usagala iliyoko mkoani Tanga Sh.500,000 baada ya mwanafunzi wa shule hiyo, Nurdin Fiomi kuibuka mshindi katika shindano la uandishi wa insha.

Pia imekabidhi Sh. 100,000 mwanafunzi huyo baada ya kushika nafasi ya kwanza mkoa.

Akizungumza baada ya kukabidhi zawadi hiyo mwishoni mwa wiki, Ofisa Habari wa AQRB, Hamisi Sungura, alisema pia shule hiyo imeshinda Sh. 300,000 kama motisha ya kuwezesha shule nyingine kuona umuhimu wa kuwashawishi wanafunzi wao kushiriki mashindano hayo kila yanapotangazwa

Sungura alisema lengo la mashindano hayo ni kuwahamasisha wanafunzi kuzijua taaluma za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

Alisema wanafunzi wengi wamekuwa wakizichanganya taaluma hizo na ile ya uhandisi, hivyo kutokana na hali hiyo, AQRB imekuwa na programu mbalimbali zinazohusisha utoaji wa elimu wa taaluma hizo ikiwa ni pamoja na kuandaa mashindano ya uandishi wa insha.

"Kwa kipindi cha mwaka 2022/23 tulipokea zaidi ya insha 500 kutoka shule mbalimbali zilizoko Tanzania Bara ikiwapo Shule ya Sekondari Usagala na Tanga Ufundi na kupata washindi wa kitaifa na mkoa ambao tunawapatia zawadi zao kupitia wakuu wa shule hizo ili wawafikishie wanafunzi wao," alisema.

Ofisa Udhibiti wa AQRB, Angel Michase alisema zawadi zinazotolewa ni motisha ya kuwavutia wanafunzi wengi kupenda kusomea taaluma hizo ambazo zinaendana na mtaala mpya wa amali.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Usagala, Alex Birumo, aliipongeza AQRB kwa kuona umuhimu wa kuandaa mashindano hayo na kuahidi kuendelea kuwashawishi wanafunzi wake kushiriki mashindano yajayo.

Mkuu wa Shule ya Tanga Ufundi, Mackmaster Luzilo, alishukuru AQRB kwa kukabidhi zawadi za ushindi kwa mwanafunzi wao na shule na kuahidi kuendelea kuhamasisha wanafunzi wa kushiriki.

# Silaa aingilia kati mgogoro wananchi, mfanyabiashara

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ameahidi kumaliza mgogoro wa wananchi 32 wa Unga Limited, jijini Arusha, ambao makazi yao yalibomolewa kwa madai ya kuvamia eneo la mfanyabiashara, Dominic Kavishe.

Nyumba hizo zilibomolewa mwaka jana baada ya mfanyabiashara huyo kudai kuwa eneo hilo ni mali yake na waliokuwa wanaishi hapo walishalipwa fidia na kutakiwa kuhama.

Akizungumza katika wiki ya kliniki ya siku saba ya ardhi inayoendelea mkoani Arusha, Silaa, alisema kuna namna ambayo haikutendeka sawa sawa, kufikia uamuzi wa kuwabomolea makazi yao wananchi wa Unga Limited.

"Naagiza timu yangu kufuatilia kwa undani mgogoro huu, ninaahidi kuja na uamuzi kamili baadaye. Iko namna ambayo, kwa vyovyote maisha ya watu makini yamechukuliwa kiurahisi.


Maana mpaka kufikia kubomoa nyumba za watu, inatakiwa uwe umejiridhisha sana, lakini hapa niwapeni pole. Nimesikiliza hoja zenu, nimesikiliza wataalamu wangu hapa.

Kuna kazi kubwa ya kufanya na nitamuelekeza Katibu Mkuu wa Wizara, atume timu ya wataalamu waje wawasikilize na baada ya kukamilisha nitakuja na uamuzi juu ya hili."

Mmoja wa wakazi waliobomolewa nyumba zao, Respisius Blasius, alisema ameridhishwa na majibu ya Waziri Silaa, hivyo anaamini wanaenda kupatiwa haki yao walionyanyaswa kwa muda mrefu.

Alisema: "Leo ninafuraha sana kwa kilio changu kufika kwa Waziri Silaa, hata familia yangu leo watafurahi. Mimi nina miezi saba natangatanga mjini, sina pa kuweka familia yangu.

...Imebidi niirudishe kijijini ili niendelee kuweka mambo sawa; lakini Waziri wa Ardhi, amerudisha matumaini ya kupatikana kwa haki zetu."





# Daktari Bingwa: Shinikizo la juu la damu bado tatizo katika jamii

**Restuta Damian,** KAGERA

JOPO la madaktari bingwa wa magonjwa ya moyo kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), limefanya uchunguzi pamoja na kutoa huduma kwa wagonjwa 10,807 kutoka mikoa 13 na kubaini shinikizo la juu la damu kuwa tatizo kubwa nchini.

Hayo yamebainishwa juzi mkoani Kagera na Daktari Bingwa wa Moyo na Mfumo wa Umeme wa Moyo, Yona Gaudiye na kusema kuwa kati ya idadi hiyo wagonjwa 194 wanahitaji huduma zaidi ya kiuchunguzi upande wa magonjwa hayo ya moyo.

Alitaja sababu ya ongezeko la magonjwa hayo kuwa ni pamoja na ulaji usio sahihi, mitindo ya maisha, matumizi ya sigara, unene uliopitiliza, unywaji wa pombe uliokithiri, upungufu wa madini ya potassium na magonjwa sugu ya figo.

Aidha alisema kwa sasa jitihada kubwa zimewekwa kuhakikisha mikoa inafikiwa na huduma hiyo ili kupunguza wagonjwa wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Hajat Fatuma Mwassa alisema, Hospitali ya Rufani ya Mkoa Bukoba idadi ya wagonjwa wa shinikizo la juu la damu imeongezeka zaidi kwa mwaka 2023.

Alisema kwa sasa miundombinu imeendelea kuboreshwa hospitalini hapo pamoja na kuongezewa vifaatiba muhimu.

Baadhi ya wananchi mkoani hapa wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti walitaja ongezeko la magonjwa hayo kusababishwa na uelewa mdogo wa wananchi pamoja na utaratibu wa watu kutokwenda katika vituo vya afya kwa wakati ili kujua afya zao.

"Wamezoea kwenda kupata huduma pale tu wanapozidiwa wakati mwingine wamekuwa wakishindwa kufuata masharti ya wataalam wa afya, hivyo kuongeza idadi ya magonjwa mwilini," alisema Laurian Rutaimukilwa.

Mkazi wa Mtaa wa Kyebitembe Kata Nshambya Manispaa ya Bukoba, Immelda Emmanuel alisema kwa miaka mitatu amekuwa akisumbuliwa na tatizo la kuchoka mwili na mapigo ya moyo kwenda kasi, huku akijua kuwa ni hali ya kawaida kwa mtu anayejishughulisha na kazi za juani.

Alisema ilifika wakati anashindwa kuamka mapema na kwenda kazini, ndipo alipoamua kutafuta dawa za kienyeji ili kutibu tatizo hilo lakini hakufanikiwa.

Emmanuel alisema: "Niliona kuwa ni hali ya kawaida tatizo lilikuja pale nilipoanza kuona kila siku shida inazidi kuwa kubwa mara moyo kujaa, nashindwa kupumua vizuri ndipo nikaenda kupima na kuambiwa ninashida katika moyo, hivyo tunahitaji kufanya uchunguzi wa mara kwa mara na kufuata ushauri wa madaktari".



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Profesa Sospeter Muhongo (kulia) akizungumza katika mkutano wa harambee ya kuchangia ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Nyabaengere, Kata Musanja, mwishoni mwa wiki, huku baadhi ya wakazi wa kijiji wakiwa na kondoo kama sehemu ya mchango wa harambee hiyo. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# DC aonya wanaokwamisha mchakato Tabora kuwa Jiji

**Na Benny Kingson,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Tabora, Deusdedith Katwale amewaonya viongozi wanaokwamisha mikakati ya kuifanya Manispaa ya Tabora kuwa Jiji na kuahidi kuwachukulia hatua za kinidhamu pindi watakapobainika.

Alitoa angalizo hilo wakati wa kikao kilichowakutanisha wakuu wa idara, vitengo, watendaji na watumishi kutoka ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa lengo la kupitia mikakati ya kimaendeleo katika manispaa hiyo.

Alisema kuwa mwelekeo wake ni wa mwaka mmoja toka sasa kuhakikisha Tabora inakuwa Jiji kwa kuzingatia vigezo vyote ambavyo wanavyo, isipokuwa cha utashi wa kisiasa ambapo alieleza kuna kila sababu ya kujipanga na kushinda.

"Katika mipango yetu lazima viongozi wawe na mawazo chanya na endapo nitabaini kuna mwenzetu anatukwamisha basi nitachukua hatua japo sisemi ni ipi kwa sasa, lakini lazima kupambana ili kufanikiwa katika hili,"alisema.

Pamoja na mambo mengine alisema viongozi wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuwashirikisha wananchi kuona matakwa yao na changamoto zilizopo, kuzitafutia ufumbuzi ili kufikia malengo.

Aidha aliagiza kuundwa kwa kamati maalumu ya kudumu kufuatilia makubaliano na mafanikio yote, kusimamia, kuratibu na kufanya mchanganuo halisi wa upatikanaji mapato kuona wanakwama wapi, akisema kwa uzoefu unaonyesha mapato mengi upotea kwa njia ya mtandao.

Aidha aliwataka kurasimisha maeneo kwa kutoa hati za viwanja na mashamba na kuhakikisha manispaa hiyo yenye kata 29, mitaa 174 na vijiji 40 inaondokana na kuwa na vijiji hivyo kwa kuwa Jiji halipaswi kuwa navyo.

Mkurugenzi wa Chuo cha Tabora Polytenics, Shabani Mrutu alisema umefika wakati ambao wakazi wa mjini hapo kuunganisha nguvu zao za kuhakikisha linakuwa Jiji.

Mrutu alisema ipo haja kwa viongozi na jamii nzima kuweka msukumo, kuhakikisha majengo yaliyopo kwenye sanamu ya Hayati Julius Nyerere yanakarabatiwa, Uwanja wa Ali Hassani Mwinyi unamaliziwa ili kuendana na ujio wa Tabora kuwa Jiji.

# Kamati yakoshwa ufanisi wa mradi wa maji Butimba

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeridhishwa na ufanisi wa mtambo wa kuzalisha na kutibu maji katika Mradi wa Maji Butimba mkoani Mwanza, kupongeza jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa kufanikisha mradi huo.

Akizungumza baada ya kukagua shughuli ya uzalishaji maji inayoendelea sambamba na hatua mbalimbali za ukamilishwaji wa mradi huo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Japhet Hasunga alisema mradi huo umezingatia mahitaji ya wananchi katika eneo hilo.

"Tumefuatilia hatua zote kuanzia maji yanapochotwa katika ziwa hadi hatua ya mwisho ambapo maji safi na salama yanaruhusiwa kufika kwa wananchi. Ni hatua nzuri kwa manufaa ya wananchi wanaofikiwa na mradi huu," alisema Hasunga.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Ellen Bogohe alisema adha ya upatikanaji wa maji mkoani hapa ilikuwa kubwa, lakini kupitia mradi huo hadi kufikia Juni mwaka huu tatizo hilo litakuwa historia.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Neli Msuya alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na uzalishaji maji unaendelea, hivyo kwa sasa unafanyika uboreshaji mifumo ya usambazaji maji ili kufikia wananchi wengi zaidi kadri ambavyo mradi ulivyotarajiwa kufika.

Katika uboreshaji wa mifumo hiyo alisema wanaendelea kulaza mabomba ya kusambaza maji, pia ipo mikakati ya kuweza kuboresha huduma za maji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu mikuu ya kusambaza maji kwa kuongeza mtandao wa bomba, kujenga matangi ya kuhifadhi maji ili yaweze kufikia wananchi wengi na hasa waishio milimani.

Alitaja maeneo yatakayopokea maji kutoka kwenye mradi huo kuwa ni pamoja na Kisesa (lita milioni tano), Nyamazobe (lita milioni tano), Buhongwa (lita milioni 10), Fumagila ya Juu -Kishiri (lita milioni 10) na Usagara (lita milioni moja).


Ukurasa 12

**Mabinti wanaofunzwa stadi za maisha wanavyogeuka tegemeo jamii, familia**



Ukurasa 13

Wazazi, walezi wakijibu swali hili hawatanyanyapaa wenye ulemavu

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 26, 2024
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


Ukurasa 14

DARASA LA MITAALA MIPYA...

**Liko kisasa; elektroniki, kompyuta, video, katuni na 'gemu' zinatumika**

ELIMU

NA BEATRICE MOSES

KUELEKEA ELIMU BILA UKOMO...

# Wataaluma walipoijadili Elimu Watu Wazima ndani ya sera mpya ya elimu

MJADALA kuhusu nafasi ya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi, pamoja na mustakabadhi wake kwa maendeleo ya jamii na taifa umefanyika hivi karibuni, ukihusisha wataalamu 450 wa 'elimu bila ukomo' Tanzania Bara na Zanzibar.

Mada mbalimbali zikawasilishwa na wabobezi wa elimu nchini; mwanazuoni mstaafu wa sheria Prof. Issa Shivji (Tafakuri ya Mwelekeo na Maudhui ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi) na mtaalamu elimu, Prof. Eustella Bhalalusesa (Utekelezaji wa Elimu bila Ukomo katika Muktadha wa Sera Mpya na Mabadiliko ya Mitaala).

Pia, wakawapo mtaaluma wa sheria, Prof. Palamagamba Kabudi akijadili 'Uzoefu wa Utekelezaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Rasmi katika nchi Nyingine'.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), ndiyo waandaaji wa kongamano lililotumika kujadili ajenda hizo iliyozinduliwa Machi Mosi, 2024 na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyn Nombo, akamwakilisha mgeni rasmi, Waziri wake, Prof. Adolf Mkenda.



Darasa la Elimu ya Watu Wazima likiendelea. **PICHA: MTANDAO**

Prof. Nombo anasema, serikali imedhamiria kuhakikisha Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, pamoja na mitaala inayogusa mifumo yote ya utoaji elimu rasmi na isiyo rasmi.

"Mabadiliko yanatakiwa katika sekta ya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi, pamoja na kukuza fursa za elimu isiyo na ukomo kwa watu wote na kumjenga Mtanzania mwenye utamaduni wa kupenda kujisomea na kujiendeleza katika muktadha wa elimu bila ukomo," anasema

Anabainisha kuwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, toleo la 2023, inalenga kukuza fursa za elimu isiyo na ukomo kwa watu wote, ikimtaka kila mwananchi kujisomea na kujiendeleza katika muktadha bila ukomo.

Prof. Nombo anafafanua: "Sera hii pia inatoa msimamo kwamba, elimu nje ya mfumo rasmi itatambuliwa na watakaopitia mfumo huo, watakuwa na fursa ya kujiunga na mfumo rasmi wa elimu kulingana na vigezo vitakavyowekwa."

Mtaaluma huyo, ana ufafanuzi namna serikali imejihakikishia kushirikiana na wadau mbalimbali, kuimarisha na kusimamia afua zote zinazolenga kutoa fursa za elimu kwa walioikosa.

"Elimu ya Watu Wazima inapewa nafasi kubwa zaidi, yaani: inaandaa jamii kupata stadi za msingi za kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, stadi za maisha; na inatoa fursa ya kuwa na jamii inayojali na kuthamini elimu," anasema.

Anasema, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, inayokumbukwa ni ile ya enzi za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ilishughulika zaidi kufuta ujinga wa kusoma na kuandika.

"Hata hivyo, kwa sasa tunataka elimu ya watu wazima ilenge mabadiliko ya sayansi na teknolojia na mtazamo wa sasa, kama ulivyosisitizwa katika sera mpya ya elimu,"

"Kongamano hili litusaidie kujadili changamoto mbalimbali katika utoaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi nchini, ikiwamo taratibu mbalimbali za utambuzi na utoaji tuzo katika fani ya Elimu ya Watu Wazima," anasema.

"Pia, kuitambua kada ya elimu ya watu wazima katika mfumo wa ajira rasmi," Prof. Nombo anaendelea, akiwa na ufafanuzi kwamba, mawasilisho ya wataalamu hao, yameibua masuala muhimu ya kufanyiwa kazi kuboresha elimu ya watu wazima, hata nje ya mfumo rasmi nchini.

Mkurugenzi wa Elimu Msingi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Abdul Maulid, anasema elimu bila ukomo kwa karne ya sasa, sio 'Kusoma, Kuandika na Kuhesabu' bali inaelekeza mifumo ya kujifunza kwa namna endelevu inayonyambua.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Mabinti wanaofunzwa stadi za maisha wanavyogeuka tegemeo jamii, familia

MAJUKUMU ya familia anayotwishwa mtoto wa kike akiwa bado mdogo hasa kwa wale wanaoishi vijijini na pembezoni mwa miji, hayamuachi salama. Kuna wakati yanamtumbukiza kwenye uhusiano wa kingono ili kutunza familia.

Ni changamoto zinazoonekana kwenye familia za wakulima na wafugaji, ambao wazazi au walezi huondoka kwenda mashambani au kusaka malisho huku mtoto wa kike akiachwa kujilea na kuitunza familia. Ni mambo yanayosababisha kujikuta kwenye mahusiano mapema ili kusaka pesa hata kulazimika kupata kile kinachokosekana nyumbani kwasababu baba na mama wako mbali.

Katika mazingira hayo Hadija Hassan, Meneja Mradi wa Elimu kwa Msichana, unaotekelezwa na Shirika la Room to Read, anasema bila kuwa na elimu ya stadi za maisha kumuandaa msichana itakuwa ngumu.

"Stadi hizo zinamuandaa kukabiliana na vikwazo vilivyopo mbele yake.Kumbuka huyu ni mama wa baadaye ataendelea kuingia kwenye kundi la wategemezi, inawezekana hata akaelemewa na madeni na kuogelea kwenye bwawa la umasikini." Anaeleza.

Anasema mradi wa stadi za maisha umefikishwa katika shule za msingi na sekondari za mikoa ya Pwani na Tanga.

"Tunaamini kwamba maendeleo yanaanza na mtoto aliyeelimika na yanaweza kukua kutokana na elimu aliyoipata akiwa mdogo."Anasema Hadija.

Hapa tunamzungumzia msichana mwenye ndoto nyingi kuanzia akiwa shule ya msingi na ili kutimiza ndoto zake ni lazima apate elimu ya stadi za maisha ambayo imeandaliwa kwa hatua kumuokoa ili awe jasiri na kuhimili maisha bila utegemezi.




Baadhi ya wanafunzi wakiwa kwenye mafunzo ya ujasiriamali. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

"Tukimuangalia mtoto wa kike tunaona anazo changamoto nyingi zinamzunguka lakini pia zinakuwa sababu ya kushindwa kupata haki yake ya elimu hasa tukianza na mila na desturi, tunaona kuna ambao mila zinasababisha kuolewa wakiwa wakiwa wadogo na huko wanapitia ukatili," anasema Meneja Hadija.

Anakumbusha kuwa hedhi zinasababisha wasichana washindwe kwenda shuleni lakini wengi bado wanakosa elimu ya kujisitiri.

### STADI WANAZOPATA

Hadija anasema Room to Read inatazama stadi tano ambazo ni ushirikiano, fikra tunduizi (critical thinking), kufanya uamuzi, ustahimilivu na uongozi.

Akianza na ushirikiano anasema wanafunzi wanafunzwa kushirikiana na kila mtu kimasomo na nje ya shule wakijengewa uwezo kushirikisha watu kwenye vitu vingne vingi wakati kwenye fikra tunduizi wanaimarika kufikiri kwa kina lakini pia wanakuwa wadadisi wa mambo mengi na kuwa na ari ya kujifunza pale wasipoelewa.

Hadija anaeleza kwamba kwenye uamuzi mwanafunzi anajengewa uelewa wa kushirikiana na wanaomzunguka na pia kuwashirikisha watu wa karibu anapoona kuna jambo linaelekea kumkatisha tamaa kufikia malengo.

"Kadhalika stadi ya Ustahimilivu hapa zipo changamoto ambazo ni vigumu kuzitafua ikiwemo ya umbali wa kwenda na kurudi nyumbani. Ni lazima aamke mapema kuwahi shule hivyo akifunzwa kustahimili inamsaidia kufikia malengo yake." Anaongeza.

Aidha, katika stadi za uongozi wasichana wanaandaliwa kuwa viongozi bora sasa na baadae wanajengwa kuelewa kuhusu stadi hiyo namna ya kujiongza wenyewe na wenzao.

"Kwahiyo tunakaa na kumfunza binti ndani ya miaka saba kumjenga, akimaliza sekondari anaendelea kujisimamia kielimu, uchumi, kifikira na kufanya maamuzi" anafafanua Hadija.

Kadhalika anabainisha kuwa mradi umeanzia shule za msingi darasa la tano na wasichana wanaendelea hadi kidato cha nne.

Anasema kupitia washauri endelevu walioko shuleni kazi kubwa ni kuwajengea wasichana uwezo kwenye stadi hizo na kuanza kuzitumia wakiwa bado wanasoma inafanyika.

Katika Halmashauri ya Mji Kibaha shule ambazo zipo kwenye mradi ni za sekondari nne na za msingi ni nne pia, kwa Pwani Room to Read imefanya kazi katika Wilaya ya Bagamoyo, Halmashauri ya Chalinze na Mkuranga.

Kwa mkoa wa Tanga mradi huo unatekelezwa katika Halmashauri za Handeni na Tanga Mjini ukihusisha shule za msingi 16, wakati Morogoro ulikuwa kwenye wilaya ya Mvomero na sasa umemalizika, Kwa ujumla Tanga, Pwani na Morogoro wasichana 5,000 wamefikiwa na kwamba 3,000 wamemaliza shule na wengine wanaendelea, anasema Hadija.

Bahati Mgala mwalimu Sekondari ya Bundikani iliyopo Kibaha, anaeleza kuwa mradi wa stadi za maisha umepunguza utoro kwa wasichana, wanajitambua na kuripoti unyanyasaji. Mgala anasema kwa wanafunzi ambao wanabainika kuwa na ufaulu hafifu kamati pamoja na walimu walio ndani ya mradi wanawatembelea nyumbani kujua vikwazo, kuvijadili na wazazi na kuvitatua.

Pamoja na kuinuka kwenye ufaulu ni wajasiriamali wanatengeneza sabuni za maji na mazulia na kuzionyesha kwa wazazi na wadau wengine wanaoalikwa kushiriki kwenye warsha inayoandaliwa kila mwaka.

### MAARIFA POPOTE

Mwajuma Yahaya (16) ni mmoja wa wanafunzi wanufaika kutoka Sekondari Bundikani, anayesema mradi huo umewakomboa kwa kuwapatia maarifa ya darasani, nyumbani na ndani ya jamii.

Anasema akisoma anaelewa, anajiamini na pia anao ujasiri kukabiliana na vikwazo tena anajiamini kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Mama mzazi wa Mwajuma mkazi wa Mailimoja Ashura Hamis anasifu juhudi za Room to Read kwa kuleta mradi huo anaosema kwasasa mtoto wake amekuwa mtunzaji wa fedha anayompatia kwa ajili ya matumizi ya shuleni na nyumbani.

"Nikikosa fedha wakati mwingine Mwajuma anatumia akiba yake. Pia ujasiriamali wa kutengeneza sabuni na mazulia anaofanya ni muarobaini wa umasikini, hatukosi vihela kidogo kujikimu." Anasema Ashura.

## Wataaluma walipoijadili Elimu Watu Wazima ndani ya sera mpya ya elimu

INATOKA UK.11

Hapo anajumuisha sehemu tatu muhimu, ambazo ni: Mfumo Rasmi wa Elimu; Elimu Nje ya Mfumo rasmi; na Elimu ya Watu Wazima.

Anaeleza umuhimu wa elimu bila ukomo, kwa sababu ya mabadiliko yanayoendelea kila wakati, ikihusisha pia uwezo wa kumudu stadi za karne ya 21, ambazo ni: za Kisomo, Kujifunza, na Maisha.

### MKUU WA TEWW

Mkuu wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Profesa Michael Ngumbi, anasema tayari wanatekeleza elimu bila ukomo na wameandaa kongamano kuiwezesha taasisi hiyo kutoa elimu kwa namna bora. kutokana na matakwa ya mahitaji ya sasa.

Anasema, pia wataalamu wamejadili maboresho ya sera na mafunzo, nafasi ya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi, mtazamo wa kisheria kuhusu elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi.

Mengine anayataja ni kushirikishwa wadau kutekeleza elimu bila ukomo, uzoefu wa elimu bila ukomo kutoka nchi nyingine, na utekelezaji elimu bila ya ukomo katika muktadha wa sera mpya ya elimu.

Mwenyekiti wa Baraza la Usimamizi la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dk. Naomi Katunzi, anatumia nafasi hiyo kuipongeza taasisi yake, kuunga mkono jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha Watanzania wote wanapata elimu bora.

ELIMU
NA ROMANA MALLYA

# Wazazi, walezi wakijibu swali hili hawatanyanyapaa wenye ulemavu

"KAMA watoto wote wenye ulemavu wangefichwa, hawa walioko wanaoifanyia nchi mambo makubwa wangetoka wapi?"

Ni swali la Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Profesa James Mdoe, akilielekeza kwa jamii yenye mtazamo hasi wa kuwanyanyapaa watu wenye mahitaji maalumu.

Ulemavu ni hali ya kimwili au kiakili ama upungufu wa kimaumbile unaomkwamisha au kufanya iwe vigumu zaidi kwa anayeishi na ulemavu kuimudu dunia inayomzunguka.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kuwa watu wanaoishi na ulemavu ni asilimia moja ya jumla ya watu wote katika taifa linalohusika.

Kwa mfano Tanzania yenye watu milioni 61 wanaoishi na ulemavu ni asilimia moja, dunia inaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu au Siku ya Walemavu Duniani kila mwaka Desemba 3.



Naibu Katibu Mkuu, James Mdoe akifungua baadhi ya vifaa vya kusaidia wenye ulemavu. **PICHA: ROMANA MALLYA**

Zipo ripoti za kuwaficha watoto, kutokana na imani zinazohusisha uelewa mdogo kuhusu kundi hilo, wengine wakiuhusisha na mikosi hata laana na kusababisha baadhi ya wazazi na walezi kuwaficha ndani. Hatua hiyo inawanyima haki muhimu kuanzia elimu, kuchangamana, kutumia vipaji vyao na kuendeleza maisha yao.

Ili kukabiliana na imani hiyo Profesa Mdoe, anasema inahitajika elimu kwa jamii ili kufuta dhana potofu iliyojengeka dhidi ya wenye ulemavu.

Anapinga vikali tabia ya baadhi ya familia wanaowafungia ndani watoto wao wenye ulemavu badala ya kuwapeleka shule kuchangamana na wenzao pamoja na kusoma. Anayasema hayo akiwa Pugu Sekondari, jijini Dar es Salaam, ambayo inatoa elimu jumuishi kwa kuwaweka pamoja wanaoishi na ulemavu na wenye viungo vilivyokamilika.

Naibu Katibu Mkuu Mdoe ambaye amesoma Pugu, anashuhudia vipaji walivyonavyo watoto hao, huku baadhi wakieleza kuwa ndoto zao ni kuwa marubani.

"Mmesikia wenyewe kwamba wengine wanataka kusoma hadi kuwa rubani, kama mzazi angemficha ingekuwaje, unadhani nini kitaendelea kama siyo kumharibia ndoto zake.

"Sasa iwe mwanzo na mwisho kwa wanaofanya vitendo vya namna hii. Nitoe wito wazazi na walezi kuona umuhimu wa kuwapeleka watoto shuleni kwani tumeshuhudia wenyewe hapa, wenye ulemavu wana vipaji tena vikubwa," anaonya kiongozi huyo.

Profesa Mdoe anafika Pugu kuzindua ugawaji wa vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum uliofanyika pia Dodoma na Jangwani, anaahidi kuzifikisha changamoto zinazokabili kundi hilo ili kupatiwa ufumbuzi.

Baadhi ya vifaa vilivyotolewa na wadau mbalimbali ni pamoja na viti mwendo 120, magodoro 26, kompyuta mpakato (laptop) mbili kwa walimu wasioona.

"Tunatambua changamoto mlizonazo na tunaendelea kuzishughulikia, lakini hapa tumepata taarifa ya viti mwendo kuwafikisha maeneo mbalimbali ikiwamo maabara, hili tumelichukua na kwenda kulifanyia kazi," anasema Prof.Mdoe.

Kuhusu wanafunzi wa elimu maalum na ufinyu wa bajeti kiongozi huyo anaeleza kuwa mazungumzo yake yanaendelea, lakini akisema changamoto hiyo haiwezi kuisha moja kwa moja bali itapungua.

Kuhusu walimu wa kufundisha elimu maalum, anasema jambo hilo linashughulikiwa kwa kuwa wanatakiwa kuwa na elimu jumuishi ikiwamo lugha ya alama.

Mkuu wa shule Boniface Orenda, anasema:"Naungana na kiongozi wangu kuwa, watoto hawa wasifichwe, tunawapokea na kuwafundisha vizuri huku tukiendelea kubaini vipaji vyao taratibu."

Orenda anasema watoto hao wanapoingia katika mfumo wa elimu kujisikia vizuri na kuona hawabaguliwi, wamekihakikisha kuwa watoto hao wanapata huduma muhimu kama za wasio na ulemavu.

"Ninashukuru uongozi mzima wa serikalini na wadau walioguswa na kutoa misaada hii kwa watoto wenye ulemavu hapa Pugu pamoja na shule nyingine," anashukuru.

Orenda anasema wana walimu wanaofundisha elimu maalum ambao wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanafunzi hao wanajifunza masomo yote na kwa muda uliopangwa.

"Kwa mantiki hii, ninampongeza Rais Samia Suluhu Hassan. Kwetu hii ni heshima kuendelea kuona umuhimu wa kutumwagia misaada katika shule yetu, japo bado tunazo changamoto chache," anabainisha.

Anasema shule hiyo ina wanafunzi wenye mahitaji maalum 139 ambao wameendelea kuhudumiwa vizuri kupitia misaada inayotolewa na Rais Samia na kuna walimu 67 kati yao, 40 ni wa kike.

> Tunaendelea kuwafikia watoto wenye ulemavu mahali popote walipo hii ni katika kuhakikisha watoto hawa wanakuwa kwenye malezi mazuri, salama na kupata elimu bora.

Mkuu wa Shule anaendelea kushukuru wadau akisema:"Tunawashukuru wadau wote ambao wamekuwa wakiona umuhimu wa watoto wetu hawa na kutusaidia ikiwamo Taasisi ya CCBRT, LM International, Kampuni ya Sigara ambayo iliyotoa kompyuta kwa wasioona."

Orenda anataja baadhi ya changamoto zilizoko shuleni hapo kuwa ni miundombinu chakavu na kusifu kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wamekuwa wakifanya vizuri sana kwenye mitihani yao na kueleza ulazima wa kuwaboreshea miundombinu pamoja na vitimwendo, daipaz za wakubwa, mashine za kufulia, miwani pamoja na kofia kwa watu wanaoishi na ualibino.

"Watanzania na wazazi watoto wenye mahitaji maalum mtambue kuwa taasisi yetu inawapokea na pia timu yangu shuleni hapa imejipanga vizuri katika kuhakikisha inabaki na daraja la kwanza na la pili na siyo la tatu na la nne kwenye ufaulu na kuwajali wenye mahitaji maalumu," anasema.

Dokta Magret Matonya, ni Mkurugenzi Elimu Maalum katika Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia elimu maalum ya watoto wanaoishi nyumbani, anasema serikali haitaacha kuwasaidia watoto hao.

"Tunaendelea kuwafikia watoto wenye ulemavu mahali popote walipo hii ni katika kuhakikisha watoto hawa wanakuwa kwenye malezi mazuri, salama na kupata elimu bora.

"Wadau wamekuwa wakijitahidi kujitokeza na kutupa misaada mbalimbali, lakini ninapenda niseme hapa mbele yenu kwamba, Mkuu wa Shule ya Pugu 'Orenda' ni jembe, kwani wakati wowote anapohitajika anapatikana na kutoa ushirikiano, hivyo kuna haja ya kumpa pongezi," anamsifu.

Desemba 1948, Umoja wa Mataifa (UN) ulipitisha azimio kwamba, binadamu wote wamezaliwa huru wakiwa sawa katika haki na kustahili heshima bila kujali upungufu wowote wa kimaumbile.

Kwa kadri ya azimio hilo, binadamu ana haki ambazo anastahili kuzipata kutoka kwa jamii na pia, ana wajibika kwa jamii.

Haki hizo ni za kuitumia jamii na rasilimali zake kwa ajili ya maendeleo na usalama wake. Kwa kuwa, mtu mwenye ulemavu ni binadamu naye ana haki hizo pia.

ELIMU
NA HALIFAN
CHUSI

DARASA LA MITAALA MIPYA...

# Liko kisasa; elektroniki, kompyuta, video, katuni na 'gemu' zinatumika

WANAFUNZI wanaoanza shule mwaka huu, wamekutana na mambo mapya wakiiona kompyuta, wakijifunza Kiingereza na michezo mingi hata kuigiza sauti ya wanyama kuanzia ng'ombe hadi simba.

Ni darasa la zama za mitaala mipya na sera mpya ya elimu, ambayo watoto wa darasa la kwanza wanaanza kujifunza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), pia wakijifunza Kiingereza jambo ambalo halijawahi kuwapo.

Dokta Aneth Komba ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), inayoandaa mitaala, vitabu na kusimamia utekelezaji wa mtaala mpya, anatoa maelezo hayo anapozungumza na Nipashe kuhusu maboresho ya elimu yaliyoanza mwaka huu.

Anafafanua kuwa kwenye TEHEMA, watakuwa wanatumia vifaa vya kielektroniki kama kompyuta na vishikwambi hata televisheni kuangalia picha, katuni, michezo (game) na kujifunza ili kuwa sehemu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Anaongeza:"Tuliipindua kabisa mitaala ya zamani tukaweka mambo mapya yanayoendana na mabadiliko ya teknolojia duniani, kwa darasa la kwanza wanafundishwa Kingereza zamani walikuwa walianzia la tatu, kuweka TEHAMA na kuendelea kufundisha hiyo historia ya Tanzania na madili."

Anasema darasa la tatu jambo jipya lililoingizwa ni maudhui ya kufundisha programu za kompyuta kwenye somo la sayansi na limewekwa somo la historia ya Tanzania na maadili badala ya maarifa ya jamiii na pia watasoma jografia na mazingira.

Dk. Aneth anasema ni kutokana na mabadiliko ya tabianchi watoto watafunzwa na kuelimishwa zaidi kwenye mazingira, wakati zamani kulikuwa na somo la sayansi na teknolojia, wamelitoa na kubakiza sayansi na ndiyo imeanza kufundisha, programu ya kompyuta

"Kuna somo jipya linaitwa naipenda nchi yangu Tanzania ambalo limelenga kufundisha maadili ya Kitanzania, historia kwa njia ya michezo na nyimbo lengo ni kujenga taratibu uzalendo kwa watoto," anasema Mkurugenzi wa TET.



Mfano wa darasa linalofundisha TEHAMA. **PICHA: MTANDAO**

> Tumefanya hivyo baada ya majadiliano marefu, unaweza ukajiuliza darasa la pili mbona hawapo, tuliona elimu ya awali na darasa la kwanza si shida wanaweza wakaanza na mitaala mipya.

### WALIMU KUPIMWA

Katika kufanikisha kufundisha mtaala mpya, walimu wapya watapimwa kwa kufanya mtihani kabla ya kuajiriwa, ili kuwapata wenye sifa watakaoliletea taifa matokeo bora pamoja na kuondoa lawama kwa watakaokosa ajira.

Ni kwa mujibu wa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof Adolf Mkenda, katika mkutano na waandishi wa habari na wahariri, unaofanyika Dar es Salaam karibuni.

Profesa Mkenda anasema ni mpango wa serikali kuboresha maslahi ya walimu wote na kuongeza hamasa na motisha mpaka pale watakapostaafu.

Anasema kuweka utaratibu wa kuwapima kwanza walimu kabla ya kuwaajiri kunatokana na wingi wa uhitaji wa ajira katika sekta hiyo.

"Ukienda sokoni walimu ni wengi kwa hiyo ukitangaza ajira hapa ni vita, Watu wakisikia ajira zimetangazwa kila mtu anaomba sasa tukasema kigezo gani kitumike kama wameomba 10,000 tunahitaji 2,000 tunachaguaje hawa?".

"Tukaona tuweke utaratibu wa kuwafanyia uthamini kuwapa mitihani watakaofaulu wataajiriwa ukiona umekosa unaweza kukata rufaa ili mtihani wako usahihishwe tena hii itaondoa kelele za kuulizwa ajira za walimu" anasisitiza Profesa Mkenda.

"Kinyume na utaratibu huo, tunakwenda kuua elimu, hata wanaosoma masomo mengine hupitia hatua hiyo kabla ya kuajiriwa.Wanaosoma sheria tunawapa mtihani wanafanya wakifaulu wanaingia kwenye ajira.Kadhalika udaktari pia.Tunawapa mtihani wanafanya wakifaulu wanapata ajira."

Anawaambia wanahabari kuwa wapo walimu waliosoma nje nafasi zikiwapo watachujwa kwa uwezo wao ili wapate ajira, akiongeza kuwa suala hilo linaleta zogo ndiyo maana analizungumzia kuondoa mkanganyiko.

Anasema kwa mwaka huu tayari imeanza mitaala mipya kwa kwa elimu ya awali, darasa la kwanza na la tatu, elimu ya sekondari kidato cha kwanza kwa shule zenye mkondo wa amali au ufundi vyuo vya elimu na kidato cha tano.

"Tumefanya hivyo baada ya majadiliano marefu, unaweza ukajiuliza darasa la pili mbona hawapo, tuliona elimu ya awali na darasa la kwanza si shida wanaweza wakaanza na mitaala mipya.

"Na wale wa zamani wa darasa la pili wakiingia la tatu pia wataendelea na elimu ya mitaala mipya, wakati wa la tatu wakiingia la nne wataendelea na elimu yao mpaka darasa la sita, mwaka 2027.Watakuwa darasa la sita kwakuwa mitaala mipya elimu ya msingi ni miaka sita si saba." Anafafanua Waziri Mkenda

### ELIMU YA LAZIMA

Waziri Mkenda anaeleza kuwa baada ya masomo wataanza kutekeleza mpango wa kutoa elimu ya lazima kwa miaka 10 akifafanua kwamba itakuwa miaka sita kwa shule ya msingi na minne kwa sekondari.

"Tukianza kutekeleza mpango huo tutawabana wazazi na walezi kuwa ni lazima mtoto amalize kidato cha nne na si vinginevyo."

Kuhusu elimu ya Sekondari, Profesa Mkenda anasema imegawanyika katika mikondo miwili elimu ya amali au ufundi na jumla akifafanua kwamba:

"Elimu ya amali itakuwa inawekeza zaidi katika mafunzo ya kazi na ujuzi mabalimbali zaidi wakati elimu ya jumla itawekeza katika masuala ya kitaaluma kama ilivyo sasa lakini itaongezwa na ujuzi kidogo" anafafanua Prof Mkenda.

### MABADILIKO

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Atupele Mwambene anasema mabadiliko yaliyoko katika mfumo huo, yatamwezesha kila Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali kitaaluma na kitaalamu.

Anasema yanatoa fursa mbalimbali za elimu na mafunzo ili kuwa na elimu na ujuzi wenye viwango vya ubora unaotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mwambene anasema utawezesha kuwa na rasilimali watu ya kutosha na yenye umahiri na weledi kuendana na vipaumbele vya taifa, usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini.

Anasema pia ni ili taifa liwe na mfumo endelevu wa kugharamia elimu na mafunzo, pia unaozingatia masuala mtambuko, ikiwamo elimu ya afya ya mazingira, magonjwa na majanga.

Kuhusu elimu ya ualimu, Mkurugenzi wa Sera na Mipango anasema itaanza kutolewa kwa wahitimu waliomaliza kidato cha sita na kuendelea na yatakuwa na mwendelezo wa kitaaluma na kitaalamu kati ya ngazi moja na nyingine.

Mafunzo chini ya uangalizi, mafunzo ya ualimu kujumuisha mwaka mmoja wakati ya chini ya uangalizi (internship) baada ya kuhitimu mafunzo tarajali (preservice training).

Anasema somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili litaanza kufundishwa kuanzia awali hadi vyuo vikuu kwa Kiswahili kwa lengo la kujenga na kuendeleza maadili, mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania.



## Daraja lililokatika mwaka 2022 kwa mafuriko lajengwa

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imekamilisha ujenzi wa daraja linalounganisha kata mbili za Minyughe na Makilawa wilayani Ikungi mkoani Singida, lililokatika miaka mitatu iliyopita.

Kukamilika kwa daraja hilo la chuma lenye urefu wa mita 30 na kuigharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni 1.6 kutafungua shughuli za kiuchumi na upatikanaji wa huduma za kijamii, ikiwemo afya na elimu kwa wanafunzi.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mkoa wa Singida, Ibrahim Kibasa, alisema wakati wa kuunganisha vyuma vya daraja hilo kutawezesha Mto Minyughe kufunguka na hivyo kutoa fursa kwa shughuli za usafirishaji kuendelea kati ya vijijini na maeneo mengine ya wilaya na mkoa.

Kibasa alisema kuwa sasa wananchi wa kata tatu zinazounganishwa na daraja hilo wataweza kuzikabili changamoto mbalimbali zilizokwamisha shughuli zao hususani wakati wa masika.

Alisema: "Sehemu ya fedha hizo mwaka huu tumejenga madaraja ikiwemo daraja hili la Minyughe, daraja hili limekuwa likiwasumbua wananchi takribani miaka mitatu na hivyo kukwamisha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa kata tatu pamoja na mkoa jirani wa Tabora, katika Wilaya ya Uyui".

Aidha, Kibasa alisema, ujenzi wa daraja hilo umetokana na bajeti iliyotengwa ya Sh. bilioni 4.4 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja, katika halmashauri ya wilaya hiyo.

Baadhi ya wananchi akiwemo, Elizabeth Bakari wa Kijiji cha Minyughe na Diwani wa Kata Minyughe Nelson Kiwesi walishukuru serikali kwa mradi huo wakisema unakwenda kuondoa adha ya usafiri hasa kwa wajawazito.

Alisema, awali iliwalazimu kukosa huduma muhimu ikiwemo za afya katika kituo cha afya kilichopo ng'ambo ya pili, pia watoto wao kuhatarisha maisha wakati wa kwenda shule hususani nyakati za masika kutokana na Mto Minyughe kufurika maji.

Pia alisema kukamilika kwa daraja hilo kutawawezesha watoto wao kupata masomo, wajawazito na wagonjwa wataenda kupata huduma za matibabu kwenye kituo cha afya kilichopo ng'ambo ya daraja hilo pamoja na kufungua shughuli za usafirishaji wa mazao na watu.

Mhandisi Mshauri kutoka TARURA, Ebenezer Mollel, alisema daraja hilo ni la tatu kujengwa hapa nchini, likitanguliwa na mengine lililopo Kihansi, huko Kilombero na lile la Mbuchi, kule Kibiti, mkoani Pwani.

# Pato la Taifa laongezeka kwa 5.3%

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, amesema katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2023, pato halisi la Taifa limeendelea kuongezeka hadi Sh. trilioni 109.2 kutoka Sh. trilioni 103.7 kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.3.

Dk. Chuwa alibainisha hayo jijini hapa alipokuwa akizungumzia utekelezaji wa shughuli za kitakwimu katika miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema pia katika kipindi hicho shughuli za fedha na bima ziliendelea kukua kwa kasi ya asilimia 16.0.

"Maana yake ni kwamba mikopo na dhamana imeendelea kuongezeka na mzunguko wa fedha katika shughuli za kiuchumi ni amani kubwa kwa wananchi wengi hususani wajasiriamali kuwezeshwa zaidi kuendesha biashara zao na miradi ya kielelezo ya Taifa kutekelezwa kama ipasavyo,"alisema.

Alisema Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, serikali imeridhia utekelezaji wa miradi miwili mikubwa ambayo imetekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Pia alisema kuwa utofauti mwingine wa sensa hiyo unatokana na matumizi ya teknolojia za kisasa katika utekelezaji wake kuanzia utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu, zoezi la ukusanyaji na uwasilishaji wa taarifa, uchambuzi na usambazaji wa matokeo ya sensa.

Alisema jambo la kujivunia kama Taifa ni kuwa katika matumizi hayo ya teknolojia za kisasa, mifumo yote iliyotumika ilitayarishwa kwa ushirikiano wa wataalamu wa kitanzania kutoka sekta ya umma na binafsi.

Alisema: "Aidha, matumizi hayo yaliwezesha Tanzania kutoa matokeo ya sensa ya sita ndani ya muda wa siku 45 tangu ukusanyaji wa taarifa Agosti, 2022 hadi uzinduzi wa matokeo ya mwanzo Oktoba 2022".



Baadhi ya wanachama wa Shirika lisilo la kiserikali la Akili Platform Tanzania (APT), wakiwa na miche ya miti, kwa ajili ya kupanda kwenye eneo la Shule ya Msingi Makole, Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali yamshikilia mwanafunzi aliyeng'atwa na nyoka Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Minandi iliyopo wilayani Ikungi mkoani Singida, Felista Charles (16), ambaye aling'atwa na nyoka amezuiwa kutoka katika Hospitali Teule ya Makiungu kutokana na kushindwa kulipa deni la Sh. milioni 1.3.

Mwanafunzi huyo aling'atwa na nyoka mguni Januari 24, 2024 wakati akilima shambani kwa mwalimu mmoja wa shule hiyo anayefahamika kwa jina moja la Robert baada ya kupewa adhabu ya kufanya kazi katika shamba hilo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, mama mzazi wa mwanafunzi huyo, Sisilia Neriko, alisema wameruhusiwa tangu Machi 21, 2024 baada ya hali ya mgonjwa kuwa nzuri lakini uongozi wa hospitali hiyo umewazuia wasitoke hadi walipe deni hilo.

"Tangu tulivyoruhusiwa Alhamisi ya wiki iliyopita leo/jana (Jumatatu) ni siku ya tano kwa hiyo gharama zitakuwa zimeongezeka tena kwasababu gharama za kulala kwenye kitanda ni Sh.3,000 na kusafisha kidonda Sh.4,000,"alisema.

Neriko alisema deni walilopewa baada ya kuruhusiwa lilikuwa ni Sh.milioni 1.8 lakini Mkuu wa Shule ya Sekondari Minandi Machi 21,2024 alitoa Sh.500,000 na kuahidi kuwa kiasi kilichobaki Sh.milioni 1.3 kitalipwa siku itakayofuata (Machi 22) lakini hadi sasa hazijalipwa.

"Mkuu wa Shule aliniambia wataenda kukaa na bodi ya shule waangalie namna watakavyolipa fedha hizo, lakini kila nikimpigia simu yake inaita tu hapokei kwa hiyo tumeendelea kukaa hapa hospitali hadi sasa na sisi uwezo wa kulipa fedha hizo hatuna,"alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Minandi, Juma Maatu, akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu alikiri mwanafunzi huyo kuendelea kuzuiliwa katika hospitali hiyo.

Alisema suala la kulipa fedha zilizobaki linashughulikiwa na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

Alisema: "Ni kweli mwanafunzi bado yupo hospitalini sisi kama shule tulipeleka Sh.500,000 na tukawaomba wazazi nao wachangie kiasi fulani gharama hizo lakini suala hili hivi sasa linashughulikiwa na ofisi ya Mkurugenzi".





# Watafiti waeleza chanzo cha konokono kushambulia mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATAFITI wa wadudu wamesema ongezeko la konokono wanaoshambulia mazao katika mikoa ya Mbeya na Songwe, limesababishwa na mabadiliko ya tabianchi pamoja na matumizi holela ya viuatilifu mashambani.

Watafiti hao kutoka katika Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI), waliyasema hayo mwishoni mwa wiki walipoambatana na maofisa wa Bodi ya Kahawa nchini kutoa elimu kwa wananchi mbinu za kuwadhibiti wadudu hao.

Konokono hao wanadaiwa kushambulia mazao mbalimbali ikiwemo kahawa, maharage, mahindi na alizeti katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe.

Mtafiti wa wadudu kutoka TaCRI, Aden Mbuba alisema wadudu hao waligundulika tangu mwaka 2019 katika mikoa hiyo na kwamba walianza kufanya utafiti wa kubaini chanzo cha ongezeko na njia za kukabiliana nao.

Alisema katika utafiti huo walibaini kuwa mabadiliko hayo ya tabianchi yamesababishwa na uharibifu wa mazingira na ongezeko la joto duniani hali inayochochea wadudu hao kuzaliana kwa kasi.

"Kwa sasa tumekuja na mbinu mbalimbali za kuwakabili wadudu hawa ili wasiendelee kuharibu mazao, tumekuja kuwafundisha wakulima kwa nadharia na vitendo lakini pia tunawapatia vipeperushi ambavyo vimeeleza vizuri mbinu hizo," alisema Mbuba.

Alizitaja mbinu ambazo wamewafundisha wakulima kuzitumia kuwa ni pamoja na kuzingatia usafi kwenye mashamba kwa kufanya palizi mara kwa mara na kuwaokota na kuwateketeza kwa kutumia chumvi ama povu la sababuni mara mbili kwa wiki.

Mbuba alitaja mbinu zingine kuwa ni pamoja na kugeuza matandazo mara kwa mara ili kuyaweka mayai ya konokono na konokono wenyewe kwa ajili ya kuliwa na wadudu ama wanyama ama kuweka mpaka wa majivu, chokaa, chumvi ama mbolea.

Meneja wa Bodi ya Kahawa Kanda ya Mbeya, Sijali Elius alisema uvamizi wa wadudu hao kwenye zao la kahawa umeanza kutishia malengo ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo kutofikiwa ama kuchukua muda mrefu kufikiwa.

Alisema lengo la serikali kwa sasa ni kuongeza uzalishaji wa zao hilo kutoka tani 80,000 za sasa mpaka tani 300,000 kwa mwaka na kwamba ndio maana uwekezaji kwenye pembejeo pamoja na wataalamu umeongezeka.

Alisema endapo wadudu hao hawatadhibitiwa kwa wakati kuna uwezekano uzalishaji wa zao hilo ukashuka zaidi na hivyo kushusha uchumi wa wakulima.

Alisema pamoja na uvamizi wa wadudu hao lakini wanawashauri wakulima wasitumie viuatilifu ovyo ili kutoharibu ubora wa zao hilo ambalo kwa zaidi ya asilimia 93 linauzwa nje ya nchi.

"Wenzetu wana teknolojia za kisasa za kupima masalia ya sumu kwenye mazao yote wanayonunua, sasa tunawashauri wakulima wetu watumie mbinu hizi wanazofundishwa na wataalamu badala ya kutumia viuatilifu vya aina yoyote," alisema Elius.

Baadhi ya wakulima walisema wadudu hao wamekuwa tishio kwenye mazao yao wakidai kuwa wamekuwa wakishambulia kwa kasi kubwa mazao hayo.

Mmoja wa wananchi hao, Godwin Mwantapila alisema mbinu ambazo walifundishwa na wataalamu zitawasaidia kutokomeza wadudu hao na kuokoa mazao ambayo yanavamiwa.



Mtoto Shamsa Ally wa darasa la kwanza Shule ya Msingi Lukooni, jijini Dar es Salaam, akijisomea huku mama yake Salma Kambi (kushoto), akimshuhudia, katika soko la Gongo la Mboto, mwishoni mwa wiki. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## 379 wagundulika kuwa na TB, DC atoa tahadhari

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa katika Halmashauri ya Mji Njombe wagonjwa 379 walibainika kuwa na ugonjwa wa kifua kikuu (TB) mwaka 2023, kati yao 135 walikuwa na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) sawa na asilimia 36.

Hayo yalielezwa na Mratibu wa kifua kikuu Halmashauri ya Mji Njombe, Dk. Mashaka Kisulila wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani yaliyofanyika mjini hapa.

Kisulila alisema kwa mwaka 2023 waliwekewa lengo lakuwafikia wagonjwa 333 na walifanikiwa kuvuka lengo hilo kwa asilimia 113.8.

"Tulifikia wagonjwa wa kifua kikuu wapatao 379 kati ya wagonjwa 1,650 waliobainika kuwa na ugonjwa wa kifua kikuu na kuwaanzishia matibabu," alisema Kisulila.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alisema wananchi wanapaswa kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa huo ambao umekuwa ukisumbua mamia ya watu nchini.

"Tuweze kushirikiana kama jamii kwanza kuzifahamu athari za kifua kikuu kwa sababu ni wengi ambao wanasikia kifua kikuu lakini hawajui athari ya kifua kikuu, hivyo naelekeza kuweka mabango kuonyesha mtu wa kifua kikuu anaonekanaje," alisema Kasongwa.

Kasongwa alisema kuwa kwa wale wenye maambukizi ya VVU waudhurie kliniki kwa wakati ili kuweza kujikinga na maambukizi mapya.

Alibanisha kwamba kwa mujibu wa Utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonesha mwaka 2021 Tanzania ilikuwa na wagonjwa wakifua kikuu 133,000 hivyo ni muhimu kwa kila mwananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Kuruthum Sadick aliwakumbusha wananchi kuwa na utamaduni wa kupima afya ili kuepuka madhara makubwa yatokanayo na magonjwa mbalimbali mwilini.

# 12,158 wanaishi na maambukizi ya VVU Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

WANANCHI 12,158 wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, wanaishi na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) huku nusu yao wakiwa ni vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 na 24.

Mratibu wa UKIMWI wa Halmasahauri ya Rungwe, George Mashimba alisema kati ya idadi hiyo ya wanaoishi na maambukizi, vijana ni 659 sawa na asilimia 5.4 huku vijana wa kike wakiwa wengi zaidi.

Alisema wasichana ni 467 huku wa kiume wakiwa 192 pekee jambo ambalo linahitaji nguvu zaidi ya kukabiliana na ongezeko la maambukizi kwa vijana.

Alisema hali ya maambukizi ya VVU katika wilaya hiyo ni mbaya na hivyo akawataka wadau mbalimbali kuungana na Serikali katika kukabiliana na tatizo hilo.

"Kutokana na hali hii naomba niwashauri vijana kujenga tabia ya kupima afya zao mara kwa mara, hii inasaidia kujiamini na kuendelea kufanya shughuli zao bila wasiwasi hata kama watakutwa na maambukizi.

Mtandao wa wanawake wanaoishi na maambukizi ya VVU Tanzania umejitosa kukabiliana na ongezeko la maambukizi hayo kwa vijana wa kike.

Mtandao huo umeanza kuwajengea uwezo vijana 12 kutoka katika vijiji sita vya Wilaya ya Rungwe ambavyo ni Kisondela, Kyimo, Isongole, Makandana na Ndanto ambao watakua mabalozi wa kutoaji elimu ya kinga.

Mkurugenzi wa programu hiyo, Veronica Lyimo alisema kupitia mpango huo watahakikisha kila kijiji kinakuwa na mashujaa wawili wanaoishi na VVU ambao watatoa elimu ya namna ya kujikinga na maambukizi.

Alisema mashujaa hao pia watakuwa wanafanya kazi ya kuhamasisha matumizi ya dawa kwa wale wanaoishi na maambukizi pamoja na ulaji wa chakula lishe kila wakati.

Veronica alisema programu hiyo itasaidia kuwafikia wasichana balehe wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo wale wanaofanya biashara ya ngono katika maeneo mbalimbali na kumbi za starehe.

Alisema watashirikiana na serikali za mitaa na viongozi mbalimbali kuhakikisha vijana wote wa kike walio katika rika balehe wanafikiwa na elimu ya maambukizi ya virusi.

"Tunataka kuwa na klabu ambazo zitakuwa chachu kwa vijana kupata elimu na kuwa huru kujieleza, tunataka kuwafikia asilimia 70 ya wanawake vijana wanaoishi na maambukizi na wale ambao wako katika hatari," alisema Veronica.

Hivyo aliwataka vijana kuhakikisha wanaishi kwa tahadhari ikiwa ni pamoja na matumizi ya kinga pamoja na kuepuka kufanya ngono zembe ambayo ni chanzo cha maambukizi.

## Serikali yajizatiti kupambana na magonjwa yasiyoambukiza

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema mikakati yake ni kuhakikisha inapambana na magonjwa yasiyoambukiza ili yasizidi kuleta athari kubwa kwa jamii ikiwemo vifo.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Afya, Khamis Hassan Hafidh wakati akipokea shehena ya dawa za kutibu maradhi ya kisukari pamoja na shinikizo la damu zenye thamani ya Sh.milioni 650 kutoka Shirika la Maendeleo la Misaada la HIPZ.

Alisema utafiti mdogo uliofanywa na Wizara ya Afya umebaini kwamba maradhi yasiyoambukiza hivi sasa yanachukuwa nafasi ya kusababisha vifo kwa wananchi wengi wa Zanzibar kuanzia watoto, vijana hadi wazee kwa asilimia 40.

Alisema kuna sababu nyingi ikiwemo mwenendo wa mfumo wa chakula uliopo sasa ambapo wananchi wengi wameacha kutumia vyakula vya asili.

Hafidh alizitaja juhudi zinazochukuliwa na Wizara ya Afya ikiwemo katika hospitali zote za wilaya zinapatikana huduma za afya pamoja na dawa kwa ajili ya kutibu maradhi yasiyoambukiza ikiwemo shinikizo la damu.

Aidha, alisema Serikali imeongeza bajeti ya sekta ya afya ili kukabiliana na tatizo la magonjwa yasiyoambukiza ambapo kuanzia vituo vidogo vya afya vinapatiwa mgawo wa dawa hizo.

Aidha alilipongeza Shirika la HIPZ kwa juhudi zake kuhakikisha inazozichukuwa kuhakikisha wananchi wanakuwa salama na masuala ya afya.

Naye Mkurugenzi wa Mipango wa HIPZ, Simon Kuhnert, alisema taasisi yake inafanya kazi katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara na kuitaja Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambayo imepewa kipaumbele katika huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

Alisema kufuatia mabadiliko ya mfumo wa maisha pamoja na chakula kwa ujumla hivi sasa kumejitokeza magonjwa mengi yasiyoambukiza ambayo yamekuwa yakisababisha vifo vingi.

Allisema wamejipanga vizuri kusaidia katika kudhibiti maradhi hayo kwa kutoa dawa zitakazotumiwa na wananchi ili kuona magonjwa hayo yanapunguwa.

Mkuu wa Bohari ya Dawa kutoka Wizara ya Afya, Abdulhamid Mohamed Mzale alisema mahitaji ya dawa hizo ni makubwa kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu wanaohitaji huduma ya matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza.

# RC aijia juu ZECO kukata umeme maeneo ya hotelini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid amesema bado kuna changamoto ya miundombinu ikiwemo umeme hafifu katika sekta ya utalii, hali inayosababisha uwapo wa malalamiko kutoka kwa wawekezaji wa hoteli na watalii.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza katika kikao cha kujadili changamoto katika sekta ya utalii kilichofanyika katika Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale mjini Zanzibar.

Alisema changamoto hiyo ya umeme mdogo husababisha hasara kubwa kwa wawekezaji wa sekta ya utalii.

"Mimi binafsi nimeshaitwa na wamiliki wa hoteli na kunionesha jinsi vyakula wanavyoweka katika friji huharibika ikiwemo vitoweo kutokana na umeme mdogo"alisema mkuu huyo wa mkoa.

Alisema hali hiyo kama haijashughulikiwa itaporomosha sekta ya utalii hasa ikizingatiwa kuwa serikali inategemea mapato kupitia sekta hiyo.

Alisema Mkoa wa Kaskazini pekee una hoteli 18 zenye hadhi ya nyota tano, hivyo tatizo na umeme mdogo utasababisha komoromoka kwa sekta ya utalii.

Aidha alisema changamoto nyingine iliyopo ni migogoro ya watalii kwa watalii ambapo imefikia hatua ya baadhi ya watalii kupigana wenyewe kwa sababu za kudhulumiana.

"Katika mkoa wangu wa Kaskazini Unguja kuna kesi kama mbili zimefikishwa ofisini kwangu ya watalii wenyewe kupigana kutokana na matukio ya kudhulumiana" alisema.

Naye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Sora alisema serikali imefanya mageuzi makubwa jambo ambalo limesababisha nchi kufunguka kiuchumi kutokana na ongezeko la wawekezaji na wageni wanaofika Zanzibar.

Alisema kutokana na ongezeko hilo lazima kutatua changamoto zilizopo ili kuongeza ufanisi hasa ikizingatiwa kuwa sekta hiyo ni sekta mama kwa uchumi na inachangia pato la taifa, ambapo asilimia 80 ya fedha za kigeni zinatokana na sekta hiyo.

Soraga alisema maeneo mengi ya kitalii ikiwemo Paje na Nungwi kuna changamoto nyingi za kiutawala ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili sekta hiyo kuendelea kupata maendeleo kwa manufaa ya jamii na taifa na kuongeza thamani ya utalii.

Aidha alisema miongoni mwa changamoto hizo ni kutokuwepo kwa uratibu na usimamizi mzuri ikiwemo ujenzi holela hadi katika fukwe, huku mamlaka husika zikichangia uwepo wa changamoto hizo kwa sababu ndizo zinazotoa vibali vya ujenzi.

Hata hivyo alizitaka mamlaka husika kuchukuwa wajibu wao katika kusimamia majukumu yao ili kurejesha nidhamu katika sekta hiyo ya utalii kwa kusimamia sheria na kanuni.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa, James Mdoe, akizunguma kabla ya uzinduzi wa mdahalo wa nane wa vijana wa Afrika Mashariki uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakala wa Barabara watekeleza agizo la Dk. Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKALA wa Barabara Zanzibar, umeanza kutekeleza agizo la Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi la ujenzi wa Barabara ya Kizimbani Dole (km3).

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kaimu Mkurugenzi Kitengo cha Utunzaji wa Barabara kutoka wakala huo, Safia Juma Ameir, alisema walipokea agizo hilo kutoka kwa Dk. Mwinyi mwaka jana katika ufunguzi wa maonesho ya nane nane.

Alisema tayari mradi huo wa ujenzi wa barabara hiyo umeanza tangu Machi 19 mwaka huu na wanategemea kumaliza ndani ya miezi mitatu.

Alisema kuwa hatua iliyopo hivi sasa ya ujenzi inakwenda vizuri na wameongeza nguvu kwa wiki nzima mpaka Jumamosi na Jumapili ili kuhakikisha ujenzi wa barabara hiyo unakamilika na kuanza kutumika kabla ya sherehe za nane.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunamaliza ujenzi wa barabara hii kabla ya sherehe za nane nane ambazo zinafanyika kila mwaka katika eneo hili," alisema.

Safia alisema barabara hiyo inajengwa kwa kutumia fedha za serikali. Alisema pamoja na uchache wa lami lakini watajitahidi wanaipata kwa wakati na kufanikisha kazi hiyo ipasavyo ambapo hadi kukamilika kwake itatumia Sh. bilioni 1.163.

Hata hivyo, alisema matarajio ya Wakala wa Barabara Zanzinbar ni kuona wananchi wanafaidika na huduma wanazotoa ikiwemo kuwawekea miundombinu nzuri na imara ili iweze kutumika kwa vizazi vya sasa na baadae.

Alisema mbali na barabara hiyo itahakikisha inaweka sawa barabara nyingine ambazo hazipitiki kwa njia ya kifusi ili kuwaondolea usumbufu wananchi hasa katika kipindi cha mvua.

Hivyo, aliwataka wananchi itakapokamilika barabara hiyo na barabara nyingine kuzitunza, kwani serikali inatumia fedha zake za ndani kwa ajili ya kuwawekea miundombinu mizuri.

Msimamizi wa mradi huo kutoka Wakala wa Barabara Zanzibar, Suleiman Issa Suleiman alisema tayari wameshaanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha kifusi na wakimaliza hatua hiyo wanatarajia kuweka lami.

Alibainisha kwamba barabara hiyo itakuwa na upana wa mita saba ambapo baadhi ya sehemu itakuwa na mita sita za lami na sehemu nyingine mita saba za lami.

Alisema kuwa hivi sasa mradi huo unakwenda vizuri na matumaini yake utakamilika kwa muda uliopangwa ili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo na maeneo jirani wanatumia barabara hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MENGSEN H SHANGALI** anatangaza kupotea kwa CHETI CHA CHUO CHA DIPLOMA kilichotolewa na TUMAINI UNIVERSITY chenye usajili namba **TU/DARCO/DBAM/017/067** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/UBU/45376/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAMAS SIRIL SAMKI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0635/0022** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MSUFINI SECONDARY SCHOOL mwaka 2005. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/KIN/45011/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AHMED ABDALLAH KINYUNYU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA** yenye usajili namba **T 572 CJM.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**MKO/RB/616/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YAHAYA MUSTAPHA OMARI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 963 DWV** AINA YA BOXER. TAARIFA IMERIPOTIWA POLISI NA KUPEWA KUMB NA **KIG/ TR/ RB/ 181/ 2024.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ERNEST PHELICIAN SHIRIMA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI NAMBA ZA USAJILI T 317 BED AINA YA TOYOTA COROLLA RANGI YA GOLD ,CHASIS **NO.NZE1213008953,**ENGINE **NO.INZA074357.** YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/KIN/42294/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**[CAP. 117 R.E 2019]**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL.**

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made this 19th day March, 2024 by me FOIDA ALLY SANGA, a resident of Iringa Tanzania.

**WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED** as follows:

1. I absolutely renounce and abandon the use of my said former name **FOIDA SANGA** appears and mistakenly registered on my **PARASTATAL PENSION FUND [PPF]** account with No: S.09710 and my personal fund details with the **PARASTATAL PENSION FUND [PPF]** and in Lieu, There fore d assume and determine to take and use the new name of **FOIDA ALLY SANGA** as it appears on my National Identity [NIDA] details with No.19671227511090000317 in substitution names FOIDA SANGA.Un fortunately ,I have not yet been supplied with my National Identity card.
2. That the reason of abandoning the name **FOIDA SANGA** is that the same was mistakenly recorded in my account details with **PARASTATAL PENSION FUND [PPF]**
3. **AND IN PURSUANCE** of such change of name[s] as aforesaid I **DECLARE** that I shall at all times hereafter in all records ,documents and other writings and in all actions ,dealings and in all occasions whatsoever use the new name of **FOIDA ALLY SANGA** in substitution the name of **FOIDA SANGA.**
4. **AND I HEREBY AUTHORISE REQUIRE** all persons at all times to describe and address me by the new name of **FOIDA ALLY SANGA.**
5. In execution of this deed I have signed my name of **FOIDA ALLY SANGA** and have set my hand this 19th day of March, 2024.

**VERIFICATION**

That all what is stated in paragraph 1, 2, 3, 4 and 5 above are true to the best of my own knowledge.

Verified at Iringa this ...19th... Day of ...March... 2024.

FOIDA ALLY SANGA

SIGNED and DELIVERED by the said FOIDA ALLY SANGA who is known to me/ introduced to me by ......................., the later known to me personally in my presence this 19th day of March, 2024.

DEPONENT



BEFORE ME:
Name: LAZARO JOSEPH HUKUMU
Signature: ..............................
Postal Address: P.O BOX 360, IRINGA
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS/ADVOCATE

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**PETRO PAGI MALALE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za Usajili ***MC.875 CSB.*** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi.

**PHQ/SHI/KAH/1234/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**FREDY BEATUS NDENDYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC 984 BZU.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/NJO/NJO/686/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**FREDY BEATUS NDENDYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC 194 CGQ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/NJO/NJO/688/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ADOLF STEVIN MWANAKULYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 714 AAQ (HUONIAO).** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/2470/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**SARAH LAZARO KEIYA** anatangaza kupotea kwa haki hati ya kiwanja **KITALU NO. 705** NJIRO. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/ARU/5180/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI.

**MARY PETER ASSEY** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Honda yenye namba za usajili **MC 629 CBK**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo karibu nae.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/TAN/TAN/1727/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI.

**ZEPHANIAH GIDION MBATTA** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki ***(T-BETTER)*** yenye namba za usajili **MC 722 ARN,** pamoja na risiti ya manunuzi ya pikipiki t-better na funguo yake. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye.

**PHQ/MOR/MOR/6949/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HERBERT GODFREY MWAIMU** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 562 CUD.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/2408/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MICHAEL OMARY MBILINYI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 134 BXH – TVS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **MKO/RB/TR/37/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NDUGU DICKSON MWESIGWA** DISMAS ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CORONA PREMIO LENYE NAMBA ZA USAJILI **T591 DBL**, CHASSIS NO. **AT211-0137463** NA INJINI NO. **7AJ175402.** AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA **PHQ/KAG/MIS/3039/2024.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA **0767932018.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3230 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE LATE TYALE HOSSEA KIULA**

**AND**

**IN THE MATTER ON AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MAGRETH NURU TUWA**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 3rd Day of 4, 2024.

Presented for filling this 7th Day of 3, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA GEITA LILILOPO GEITA**

**MAOMBI NA 08/2019**

**DAUDI PETRO KASAMBULA..................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **VASTA ANDREA (Msimamizi wa Mirathi ya marehemu JOASH S. MPENDE)**
2. **VASTA ANDREA...........................WAJIBU MAOMBI**

Kwa **VASTA ANDREA** popote ulipo unafahamishwa kwamba mleta maombi tajwa hapo juu amefungua shauri la madai dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Geita lililopo Geita, maombi haya yamepangwa tarehe 15/04/2024 kwaajili ya kutajwa/kusikilizwa.

Hivyo basi unaamriwa kufika shaurini katika ofisi za Baraza saa 3 Asubuhi wewe mwenyewe au wakili wako au mtu yeyote aliyeruhusiwa kisheria. Nakala ya madai inapatikana katika Ofisi za Baraza.

**KAA UKIJUA** kwamba kushindwa kufika kwako, baraza litasikiliza shauri na kutoa hukumu/maamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya baraza hili leo tarehe 21/03/2024

C. KATO
MWENYEKITI
21/03/2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**

**SHAURI LA TALAKA NO 8/2024**

**EMILIANA VENTESILAUSI............................MDAI**

**NAZARETH PIRWA KAGAMO.........................MDAI**

**KUITWA SHAURINI.**

Mdaiwa **NAZARETH PIRWA KAGAMO** popote pale ulipo unatakiwa kufika mahakamani 8/04/2024 saa 2:30 asubuhi kwajili ya shauri la talaka.

Usipofika tarehe husika ,shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 25/03/2024.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO
IRINGA MJINI

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

# Mbowe: Heshima yetu yaja

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema Kanda ya Kaskazini itarejesha alichokita "heshima yake" katika Uchaguzi Mkuu ujao wa Rais, wabunge na madiwani mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji mwaka huu.

Ni kauli aliyoitoa jana alipofanya mkutano wake wa kisiasa kwa mara ya kwanza katika Jimbo la Hai, mkoani Kilimanjaro tangu alipotangazwa kushindwa katika uchaguzi wa kiti cha ubunge mwaka 2020.

Katika mkutano huo wa hadhara uliofanyika katika Viwanja vya Snow View, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, Mbowe alisema:

"Tumerudi na tumesimama kama tulivyoondoka. Tunapanga turejeshe heshima yetu kama watu wa upinzani Kanda ya Kaskazini.

Nyumbani ninakuja kufanya finishing (kumalizia), nilisema ngoja kwanza nimalize mikoa yote.

"Tunataka kulifanya Jimbo la Hai lifanane na Mwenyekiti. Tunakwenda kubeba asilimia 90 ya vijiji, vitongoji na vijiji. Nipeni madiwani wazuri, hebu kila mmoja asiwe msikilizaji, awe mtekelezaji.

"Jumatatu ya Pasaka, ninakwenda Australia. Ninakwenda kwenye mikutano ya IPU, ambayo mimi ni Mwenyekiti. Ninyi mtakuwa mnakula Pasaka, mimi nitatumia saa 36 angani.

"Tuanze kujipanga kwenye mitaa yetu, kwenye vijiji na kwenye kata," alifafanua Mbowe, pasi kutaja moja kwa moja azma yake ya kujitosa katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Godbless Lema, Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini na Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, alisema serikali imekosa sera ya uchumi dhidi ya vijana, ndio maana wameamua kuwa waendesha bodaboda, na mengine magumu yasiyofaa kwa vijana wa kike.

"Tunaibiwa kura kwa sababu hamweleweki, tumeumizwa, tumedhalilishwa, wengine tulikimbia nchi kwa sababu wananchi hawaeleweki.

"Badala ya kujadili mambo ya msingi tumeishia kwenye ushabiki wa mpira. Ukweli hakuna watu wanavunja moyo kama wananchi wa Tanzania. Hali ni mbaya, umaskini ni mkubwa.

"Ukitaka uamini hali ni mbaya, ngoja uone bufee imewekwa, watu wanavyopanga mstari na wengine kugombania. Haya mambo hatuwezi kuyarekebishia kanisani au msikitini, mambo hayo tunayafanyia kwenye mikutano kama hii.

"Vijana wengine wamekuwa walevi kwa sababu ya umaskini, wakiamka wamekata loku. Mbowe amebadili ndege, leo alikuwa anakwenda Dar kuna kikao cha ndani. Hili jimbo analitaka bingwa wa siasa za upinzani; na ni lazima liyazidi majimbo ya Arusha Mjini, Mwanza Mjini na Mbeya Mjini."

Katika mkutano huo, Lema pia alisema katika Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2025, Kanda ya Kaskazini itakuwa Kanda ya mfano kwa kurejesha wabunge na madiwani.

Awali, Katibu wa Kanda ya Kaskazini CHADEMA, Amani Golugwa alitamba: "Tumekuja kukiwasha, tumekuja kukinukisha, Hai, jimbo linatakiwa lirudi kwenye mikono ya wenyewe."

## Upinzani waongoza kura za urais Senegal

**DAKAR,** Senegal

MGOMBEA wa upinzani nchini Senegal Bassirou Faye anaongoza katika matokeo ya awali ya uchaguzi wa urais ambao ulifanyika baada ya miaka kadhaa ya ghasia na mzozo wa kisiasa.

Mshindi wa uchaguzi huo atatwikwa jukumu la kuiongoza Senegal, inayotazamwa kama kinara wa demokrasia katika eneo la Afrika Magharibi lililokumbwa na matukio ya mapinduzi, na kuiondoa katika matatizo yake ya karibuni na kusimamia mapato kutoka kwa hifadhi za mafuta na gesi ambazo zinatarajiwa kuanza uzalishaji hivi karibuni.

Sintofahamu ilitanda kuhusu matokeo ya uchaguzi huo, huku matokeo rasmi yakitarajiwa mwishoni mwa wiki na wingi mkubwa wa kura ukihitajika ili kumpata mshindi wa moja kwa moja katika duru ya kwanza.

Kiongozi wa upinzani Faye alikuwa amewaahidi wapiga kura mabadiliko makubwa na ya kweli, na kwamba kwa sasa ameonekana kupata uongozi wa mapema dhidi ya aliyekuwa Waziri mkuu wa zamani wa muungano unaotawala Amadou Ba.

Ilielezwa kuwa karibu wagombea saba wa urais kati ya 17 wamempongeza Faye kutokana na dalili za mwanzo za kura zinazoendelea kuhesabiwa. Akiwamo mgombea pekee wa kike katika kinyang'anyiro hicho Anta Ngom, aliandika kwenye mtandao wake wa X, "Hongera kwa Bassirou Faye kwa ushindi wake usio na shaka".

Mgombea mwingine Dethie Fall, alimpongeza Faye kwa ushindi wake, uliopatikana hasa kwa kuzingatia mienendo imara inayoibuka.



Mgombea wa upinzani, Bassirou Faye akifurahi baada ya matokeo ya awali ya uchaguzi wa urais nchini Senegal kuonyesha kuwa anaongoza, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Saratani yatikisa kasri la Mfalme wa Uingereza

**Na Christina Mwakangale**

KASRI la Buckingham, linapitia changamoto. Kwa kipindi cha mwezi mmoja hali ya kiafya ndani ya jumba hilo la kifalme, imetikiswa.

Vyombo vya habari vya kimataifa, Shirika la Utangazaji la Uingereza pamoja na The Guardian, CNN na vinginevyo vimeripoti kwenye tovuti zao kwa vipindi tofauti.

Mfalme Charles III (75) na mkwe wake, Bintimfalme wa Wales, Catherine (42), wanapokea matibabu katika hospitali moja, London Clinic, wakiugua ugonjwa wa saratani. CNN, imeripoti, juzi.

Bintimfalme huyo, maarufu Kate, mwishoni mwa wiki, ameuelezea umma kwamba, amegundulika anaugua ugonjwa huo, huku taarifa hizo zikipokewa kwa mitazamo tofauti hususani kwenye mitandao ya kijamii.

Kadhalika, mapema Februari, mwaka huu, taarifa kutoka kasri hilo, zilieleza kwamba Mfalme Charles III, ameanza matibabu ya ugionjwa huo, Februari 5, mwaka huu. Haikutajwa aina ya saratani anayougua.

"Januari (mwaka huu), nilifanyiwa upasuaji wa tumbo London na wakati huo ilifikiriwa kuwa hali yangu si ya saratani," anasema Catherine, mke wa Mwanamfalme William.

Catherine, ametangaza hilo kwa hisia, kupitia video, iliyosambazwa na vyombo vya kimatafa na mitandaoni, Februari 22, mwaka huu, mwishoni mwa wiki.

Alizungumza kupitia video hiyo kwa dakika mbili na sekunde 16. Mara kadhaa, Bintimfalme huyo, aliongea taratibu, ingawa kwa sekunde kadhaa, alitazama chini pale alipozungumzia mshtuko kwa familia yake kuhusu habari hizo.

Katika maelezo yake ya video, Catherine alisema anapokea matibabu kwa mionzi (chemotherapy), tangu Februari, mwaka huu. Taarifa hiyo imekwenda sambamba na kuutaka umma kuipa faragha familia ya kifalme, wakati huu.

Mashirika ya misaada dhidi ya saratani, London, yameusifu uwazi wa Bintimfalme huyo, ambaye yupo katika matibabu ya awali ya ugonjwa, huku viongozi wa dunia, marafiki na watu mashuhuri wakimtakia heri.

Catherine na mumewe William, wanahitaji muda zaidi, kuwaelezea watoto wao watatu, kuhusu suala hilo. Watoto wao ni; George (10); Charlotte (8); Louis (5).

"Unaweza kufikiria, hii imechukua muda. Imenichukua muda kupona kutoka...lakini muhimu zaidi, imetuchukua muda kueleza kila kitu kwa George, Charlotte na Louis, kwa njia ambayo inafaa kwao na kuwahakikishia kuwa nitakuwa sawa."

"Hii bila shaka kuna mshtuko mkubwa, mimi na William tumekuwa tukifanya kila tuwezalo kushughulikia, kudhibiti hili kwa faragha kwa ajili ya familia yetu iliyo changa," alisema akiongeza:

"Imekuwa ni miezi michache migumu sana kwa familia yetu, lakini nimekuwa na timu nzuri ya matibabu ambayo wamenitunza sana, ambayo ninashukuru sana."

Wanandoa hao wa kifalme, wataadhimisha kumbukumbu ya miaka 13 ya ndoa yao, mwezi ujao.

Mfalme Charles III na Malkia Camilla, walisema wataendeleza upendo wao na msaada kwa familia nzima katika kipindi hiki kigumu.

Muda mchache baada ya Mfalme Charles III, kutangazwa anaugua ugonjwa huo Februari, mwaka huu, alisema ataahirisha shughuli zake za umma na inatarajiwa kwamba wanafamilia wengine wakuu wa familia ya kifalme, watamsaidia shughuli zake za umma wakati wa matibabu yake.

Hakukuwa na maelezo zaidi yaliyotolewa ya hatua ya saratani au matibabu atakayopewa, ingawa ataendelea na jukumu lake la kikatiba kama mkuu wa nchi.

## HABARI MICHEZO

# ZAF YATOA SABABU ZANZIBAR KUVURUNDA ALL-AFRICAN GAMES

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Riadha Zanzibar (ZAF), limesema kufanya vibaya kwa wachezaji wao waliomo kwenye Timu ya Taifa inayoshiriki mashindano ya All-African Games, kumetokana na kukosa sehemu ya kufanyia mazoezi baada ya Uwanja wa New Amaan Complex kufungwa kwa matengenezo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, Katibu wa ZAF, Muhidini Yasin, alisema wachezaji wao huutumia uwanja huo kwa ajili ya mazoezi kujiandaa na mashindano mbalimbali, hivyo kufungwa kwa uwanja huo kulisababisha kufanya mazoezi katika viwanja vya nje visivyo na ubora kama New Amaan Complex.

**Alisema katika timu hiyo ya taifa ambayo Kocha Msaidizi, Makame Hassan Juma kutokana Zanzibar, walitoa wachezaji wawili ambao wote viwango vyao vimeshuka.**

Aliwataja wachezaji hao ni Ali Khamis Gulamu ambaye alikimbia mita mita 200 na kufika hatua ya nusu fainali na mita 100 hakuingia mzunguuko unaofuata.

Mwingine alimtaja kuwa ni Mwanaamina Hassan Mkwayu, alirusha mkuki na kushika nafasi ya tisa kati ya mataifa 54 yanayoshiriki mashindano hayo jijini Accra, Ghana.

Alisema kawaida mchezaji huyo hurusha mkuki umbalia wa mita 48, lakini safari hii alishuka kiwango na kurusha umbali wa mita 40 na mara ya mwisho aliendа kucheza Zambia mwaka jana alimaliza nafasi ya tatu.

"Viwango vyao vimeshuka kutokana na ukosoefu wa maeneo sahihi ya kufanyia mazoezi, tangu mwaka jana Mei Uwanja wa Amaan umefungwa, kwa hiyo wachezaji hawana sehemu ya kufanyia mazoezi na badala yake hufanya kwenye viwanja vya nje ambavyo havina ubora," alisema.

Aidha, aliiomba serikali kuhakikisha ukarabati wa uwanja huo unamalizika haraka ili wapate sehemu sahihi kwa ajili wachezaji wao kufanya mazoezi kuelekea michuano ya kitaifa ijayo.

Alisema ili mchezaji awe bora ni lazima afanyanye mazoezi katika njia maalum za kukimbilia ambazo ndizo wanazotumia kwenye mashindano ya kimataifa, lakini kufungwa kwa uwanja huo kunawafanya wachezaji wao kutokufanya vizuri kutokana na kushindwa kujiandaa vema kwa sababu ya miondombinu ya viwanja.

**TUPO TAYARI...**



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini katika uwanja wa nje wa New Amaan Complex, Zanzibar, kujiwinda na mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri itakayopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# Mbeya Kwanza yaibeba Pamba Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya Kwanza juzi ilitibua mipango ya Biashara United kutaka kukaa kwenye nafasi ya pili ya Ligi ya Championship, baada ya kuipa kipigo cha bao 1-0 na kuifanya Pamba FC kupumua, ikiendelea kushika nafasi hiyo.

Bao la dakika za majeruhi lililofungwa na Fredrick Magata kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara lilizima ndoto ya Biashara United yenye pointi 53, ambayo ilikuwa inasaka ushindi kwa udi na uvumba ili kufikisha pointi 56 na kuiengua Pamba yenye pointi 55.

Kwa matokeo hayo, Pamba inabaki kwenye nafasi ya pili na pointi hizo, Biashara United ikisalia nafasi ya tatu na pointi zake 53, huku timu zote zikiwa zimebakisha mechi nne kumaliza msimu wa ligi hiyo.

Kwa misimu kadhaa, Pamba imekuwa ikipigana kurejea Ligi Kuu, lakini imekuwa ikikwamia kwenye 'play off', kitu ambacho viongozi wake wamesema hawataki kukisikia msimu huu.

Baada ya ushindi huo wa bao 1-0, Mbeya Kwanza inapanda hadi nafasi ya nne ikifikisha pointi 53 sawa na Biashara United, hivyo kukoleza moto wa mchuano mkali wa timu zinazowania kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Katika ligi hiyo, mchuano mkali unaonekana ni kusaka nafasi ya pili ya kupanda moja kwa moja, huku Kengold inayoongoza na pointi 60, ikihitaji pointi sita tu kati ya michezo minne iliyosaliwa nayo ili kukwea Ligi Kuu.

Timu zitakazomaliza nafasi ya tatu na ya nne, zinacheza 'play off', kitu ambacho inaonekana timu nyingi za Champioship zinakikwepa.

**Baada ya ushindi huo wa bao 1-0, Mbeya Kwanza inapanda nafasi ya nne ikifikisha pointi 53 sawa na Biashara United...**

# *Simba yatinga nane bora U-20, Yanga nje*

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 3-2 ilioupata timu ya vijana ya Simba chini ya miaka 20 dhidi Coastal Union juzi, umeifanya timu hiyo kutinga hatua ya nane bora ya ligi hiyo inayoendelea nchini.

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa TFF Kigamboni, Simba ilitoka nyuma kwa mabao mawili na kuweza kusawazisha kabla ya kufunga la tatu lilioifanya kumaliza ikiwa nafasi ya nne kwenye Kundi A.

Katika ligi hiyo inayozikutanisha timu za vijana za klabu zinazocheza Ligi Kuu, wanaomaliza nafasi nne za juu ndiyo wanaosonga mbele kwenye hatua ya nane bora. Timu hizo zimegawanywa katika makundi mawili, kila kundi likiwa na timu nane.

Wakati Simba ikimaliza nafasi ya nne na pointi zake 20, timu ya Yanga chini ya umri huo imeshindwa kufuzu katika kundi hilo baada ya kumaliza mechi zake zote 14 ikiwa ya sita na pointi 16.

Timu zilizofuzu ni Azam FC iliyomaliza na ponti 32, Coastal Union licha ya kufungwa imefuzu ikiwa na pointi 26, Ihefu na Simba zote zikiwa na pointi 20.

Kundi B, timu zilizofuzu ni Dodoma Jiji iliyomaliza na pointi 28, JKT Tanzania ya pili ikiwa na pointi 24, Geita Gold nafasi ya tatu na pointi zake 22, huku Kagera Sugar ikifuzu kwa pointi 21, kwenye nafasi ya nne.

Timu hizo nane zitacheza hatua ya mtoano ili kupata bingwa wa Ligi ya Vijana chini ya miaka 20 msimu huu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### BRANTHWAITE ANYATIWA

MANCHESTER City wanafuatilia matukio yanayomhusu beki wa kati wa Everton, Jarrad Branthwaite, 21, huku Manchester United, Tottenham Hotspur na Real Madrid pia wakimtaka Mwingereza huyo. ***(Mail)***

#### UNITED NA MCTOMINAY

MANCHESTER United imekuwa ikihusishwa na kumuuza kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay, 27, lakini klabu hiyo inapanga kusalia na mchezaji huyo na kumpa mkataba uliooboreshwa. ***(Star)***

#### NEVES ALENGWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inamlenga kiungo wa Benfica, Joao Neves, 19, kama mojawapo ya vipaumbele vyao msimu wa majira ya joto, lakini klabu hiyo inaweza pia kufikiria kumnunua mchezaji wa Kimataifa wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 28, anayechezea Juventus, kama chaguo wanaloweza kumudu. ***(Caught Offside)***

#### WEST HAM KWA TONEY

WEST Ham inapanga kumnunua mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, 28, ambaye amehusishwa na Arsenal na Chelsea. ***(Football Insider)***

#### GALLAGHER APANDIWA DAU

KLABU ya Tottenham Hotspur inaandaa dau la mapema la msimu wa majira ya joto la kati ya pauni milioni 30 hadi 40 kumnunua kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, 24, ambaye mkataba wake na Chelsea unamalizika 2025. ***(Football Insider)***

#### BAYERN YAMSIKILIZIA DAVIES

BAYERN Munich inataka uamuzi kutoka kwa beki wa kushoto wa Canada, Alphonso Davies, 23, wiki ijayo kuhusu iwapo mchezaji huyo ambaye anahusishwa na Real Madrid, atakubali mkataba mpya. ***(Sky Sports Germany)***

#### GUDMUNDSSON KWENYE RADA

MSHAMBULIAJI wa Genoa, Albert Gudmundsson, 26, yuko kwenye rada ya Tottenham Hotspur wakati Inter Milan pia inavutiwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Iceland. ***(Football Transfers)***

#### NAGELSMANN HAONGEZI

JULIAN Nagelsmann, 36, amesema "haiwezekani" kuongeza mkataba wake kama kocha wa Ujerumani hadi mwisho wa michuano ya euro 2024 msimu huu wa majira ya joto, na mazungumzo kuhusu mkataba mpya yamefanyika. ***(Metro)***

#### FAYE ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United inaweza kujaribu kumsajili beki wa Senegal, Mikayil Faye, 19, kutoka Barcelona majira ya joto. ***(Mail)***

#### BRAZ HUYOOO NEWCASTLE

RUI Pedro Braz wa Benfica yuko kwenye orodha ya warithi wanaotarajiwa kuchukua mikoba ya Dan Ashworth kama mkurugenzi wa michezo wa Newcastle United. ***(Times)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# WALKER, MAGUIRE PIGO KUBWA KIKOSI ENGLAND

**LONDON,** England

KYLE Walker na Harry Maguire wamejiondoa kwenye kambi ya England kutokana na majeraha, Chama cha Soka cha England (FA), kimetangaza.

**Wawili hao, pamoja na kipa Sam Johnstone, watarejea katika klabu zao kwa ajili ya kufanyiwa tathmini zaidi juu ya majeraha waliyoyapata siku za hivi karibuni kwa mujibu wa FA.**

Walker, ambaye alitajwa kuwa nahodha wa England kwa mechi dhidi ya Brazil Jumamosi, alitolewa dakika ya 20 baada ya kuonekana kuumia misuli ya paja aliporejea kuokoa mpira uliotoka nje ya mstari kutoka kwa Vinicius Junior mapema katika mchezo huo.

"Hatujui ni uzito kiasi gani," alisema Kocha wa England, Gareth Southgate, akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo, ambao Brazil walishinda bao 1-0.

> ●●● Hatujui ni uzito kiasi gani, tutajua zaidi siku chache zijazo baada ya...

"Hajapata majeraha mengi kwa hiyo hana uhakika kama ni kubana tu au jambo baya zaidi. Tutajua zaidi siku chache zijazo."

Maguire alidumu hadi dakika 67 uwanjani Wembley Jumamosi, kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Lewis Dunk. Msururu wa hivi punde wa kujiondoa unatoa pigo jipya kwa Southgate, ambaye tayari amewashuhudia Harry Kane na Bukayo Saka wakiondolewa kwenye kikosi hicho siku za hivi karibuni.

Kane, ambaye alikuwa jukwaani wakati England ikicheza na Brazil Jumamosi, alikuwa amejiunga na kikosi kabla ya mchezo huo licha ya kupata jeraha la kifundo cha mguu katika ushindi wa Bayern Munich dhidi ya Darmstardt kabla ya mapumziko ya kimataifa.

Akizungumza baada ya mechi ya Jumamosi, Southgate alithibitisha kwamba fowadi huyo amerejea katika klabu yake ili kupata nafuu kutokana na jeraha lake na hatashiriki mechi ya kirafiki ya England dhidi ya Ubelgiji leo Jumanne.

Saka, ambaye kama Kane alijiunga na timu ya England kabla ya mechi za kirafiki, aliondoka kambini St.George's Park wiki iliyopita baada ya FA kutangaza kuwa amewasili akiwa na jeraha na hakuweza kushiriki katika mazoezi.

Beki wa Manchester City, Rico Lewis, ambaye alicheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Macedonia Kaskazini Novemba, na kipa wa Burnley, James Trafford wamepandishwa kutoka timu ya vijana chini ya umri wa miaka 21 hadi kwenye kikosi cha wakubwa.

# LAPORTA ATAKA XAVI ABAKI BARCELONA



**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesisitiza kwamba anataka Xavi Hernandez abaki kama kocha wa klabu hiyo baada ya msimu wa 2023/24.

Xavi alitangaza nia yake ya kuondoka Barca mwishoni mwa msimu wa 2023/24 miezi michache iliyopita kutokana na hali mbaya iliyowafanya kupoteza mechi mbili za El Clasico na kujiondoa katika mbio za ubingwa wa LaLiga.

Tangu wakati huo, kiwango cha 'La Blaugrana' hao ndani kimeimarika sana.

Barca kwa sasa wamefurahia mechi 10 bila kufungwa katika mashindano yote, na hivi karibuni walijikatia tiketi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu 2020 kwa ushindi dhidi ya Napoli.

Laporta amesema kuimarika kwa kiwango chake kumesababisha mashabiki kumtaka Xavi kubaki klabuni hapo huku taarifa zikieleza kuwa kuna masharti matatu ambayo yakizingatiwa yanaweza kumfanya kocha huyo kubaki.

Moja ya masharti yaliyosemwa inaripotiwa kuwa Barca inamtaka Xavi haswa kubadili uamuzi wake na, akizungumza katika mahojiano na Mundo Deportivo, Laporta alitoa dalili kwamba hilo linaweza kutokea:

"Ndio, ndio, ndio, ndio, tayari anajua kwamba Barca wanataka Xavi abaki, lakini anatambua. Ningependa aendelee, lakini tayari nilimwambia wakati huo, aliposema juu ya shinikizo, kwamba hapa sisi huwa chini ya shinikizo na uzoefu ulio nao.

"Nilimuuliza kama kuna njia yoyote ya kubadilisha mawazo yake, lakini nilimuona akikabiliana na presha isiyoweza kushindikana ambayo inaweza kuonekana usoni mwake, nikamwambia atulie akiona hivyo."

## Amrabat kurudi Italia

**MANCHESTER,** England

KLABU za AC Milan na Juventus zinaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa Fiorentina na Morocco, Sofyan Amrabat, ambaye kwa sasa anaichezea Manchester United kwa mkopo.

Hadi sasa Man United haijaonesha nia ya kutaka kumsainisha mkataba wa kudumu Amrabat aliyejiunga nao katika dirisha lililopita la majira ya baridi.

Amrabat alijiunga na Man United kwa mkopo uliokuwa na ada ya euro milioni tisa na kuna kipengele cha kumnunua mazima kwa Euro milioni 25.

Juventus ndio imeripotiwa kuwa ya kwanza kutaka kumsajili staa huyu, lakini Milan nayo imeibuka katika siku za hivi karibuni, na ndio inaonekana kuwekeza nguvu kubwa zaidi.

Milan inataka kumsajili Amrabat kwa sababu inapitia changamoto eneo lao la kiungo hususan katika upande wa kuzuia.

Amrabat alitua Man United baada ya 'Mashetani Wekundu' hao kushinda vita dhidi ya Barcelona. Tangu atue Mana Utd, kiungo huyu amecheza mechi 22 za michuano yote na mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwaka 2025.





## Tchouameni alia Real kumzuia kucheza Olimpiki

**PARIS,** Ufaransa

KIUNGO wa Real Madrid, Aurelien Tchouameni, ameeleza kusikitishwa na uamuzi wa klabu hiyo kuwazuia wachezaji wake waandamizi kushiriki michuano ya Olimpiki msimu huu.

Tchouameni alikuwa na mpango wa kuiwakilisha Ufaransa katika mashindano ya soka ya wanaume katika ardhi ya nyumbani kama mchezaji aliyezidi umri, huku mchezaji mwenzake, Eduardo Camavinga pia akistahili.

Kylian Mbappe, ambaye anatarajiwa kuwa mchezaji wa Madrid Julai, ni mchezaji mwingine ambaye Olimpiki ni matarajio yake.

"Ni wazi, kucheza katika Michezo ya Olimpiki, katika nchi yako, ni jambo la aina yake. Si jambo ambalo labda tunaweza kurudia katika maisha yetu, lakini Real Madrid ni mwajiri wetu," alisema Tchouameni akiwa kwenye majukumu ya kimataifa na kikosi cha Ufaransa.

"Tangu wakati Real Madrid ilipoamua, nadhani hatuna mengi ya kusema. Mbali na hilo, kila mtu anajua kwamba si lazima kutofautiana na mwajiri wako katika maisha ya kila siku. Ukweli ni kwamba tungependelea. Hilo halitawezekana lakini tutakuwa wa kwanza kuiunga mkono Ufaransa."

Katika soka ya wanaume, Olimpiki ni mashindano ya vijana chini ya miaka 23, lakini kila nchi inaruhusiwa kuchagua hadi wachezaji watatu wakubwa.

Mbappe mwenye umri wa miaka 25 na Tchouameni mwenye miaka 24, wangehesabiwa katika nafasi hiyo, huku Camavinga akiwa bado na miaka 21.

Lakini kwa kuwa wachezaji kama Lionel Messi na Neymar ni miongoni mwa wachezaji wa hadhi ya juu walioshinda medali za dhahabu kufikia sasa karne hii, inazidi kuwa ya kifahari.

Mashindano ya kandanda ya Olimpiki ya 2024 yataanza Julai 25 hadi Agosti 10, yakianza siku tisa tu baada ya fainali ya Euro 2024.

## HABARI MICHEZO

# Dabo aiandalia Namungo dawa

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Azam FC, Youssouph Dabo, ameanza kuandaa silaha zake za maangamizi kwa ajili ya mechi zilizobaki za Ligi Kuu, akianza kutafuta pointi tatu katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC.

Amesema amecheza mechi ya kirafiki dhidi ya Zimamoto FC, kupata utimamu wa mwili na kujiandaa na mechi zinazokuja kwa kuendelea walipoishia katika mechi yao ya mwisho dhidi ya Yanga ambayo walibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema mechi hiyo imemsaidia kuona mapungufu ya kikosi chake na kuyafanyia kazi kwa sababu malengo yao ni kutafuta pointi muhimu katika kila mechi.

Alisema anachoangalia ni umakini wa wachezaji wake katika kila eneo, safu ya ulinzi na ushambuliaji kuhakikisha wanatumia nafasi zinazopatikana na kutoruhusu bao.

"Hii mechi ya kirafiki ni muhimu sana, hatuangalii matokeo bali ni yale niliyowapa uwanja wa mazoezi, mikakati yangu ni kuona tunafanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu tukianza na dhidi ya Namungo FC," alisema Dabo.

Aliongeza kuwa anafurahi kuona baadhi ya majeruhi wameanza kurejea kufanya mazoezi mepesi jambo ambalo linampa matumaini ya kurejea kwa kikosi kipana.

"Majeruhi walioanza mazoezi ni beki wetu Sebo (Abdallah Kheri), ameanza mazoezi ya utimamu wa mwili, Sospeter Bajana na Navarro (Franklin) aliyetakiwa kuwa nje kwa miezi minne, ameshatumikia mwezi mmoja amebakiza mitatu kurejea uwanjani."

Azam FC wanaendelea kujifua katika uwanja wao wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, kujiandaa na mchezo wao dhidi ya Namungo FC utakaopigwa Aprili 13, mwaka huu, kwenye dimba la Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

## Pacome, Aucho fiti kuivaa Mamelodi

INATOKA UKURASA 24

Ofisa habari huyo amekiri kuwa mechi yao itakuwa ngumu, lakini amewataka wanachama na mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani ili kuipa sapoti timu yao kupata ushindi mnono ambao unaweza kuwasaidia katika mechi ya maruduano nchini Afrika Kusini.

Aidha, alilishukuru Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kwa kuwarejesha kwa wakati wachezaji wao watatu waliowahitaji kwa mujibu wa makubaliano yao.

"Kikosi kinaendelea na mazoezi, habari njema ni kwamba Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini, limewaruhusu wachezaji wetu kurejea mapema kwa ajili ya maandalizi, ambao ni Mudathir Yahaya, Ibrahim Hamad 'Bacca', na Clement Mzize tayari wapo mazoezini na wenzao, tunaishukuru sana TFF," alisema.

# SIMBA YAPIGWA FAINI, SHABIKI AFUNGIWA KUINGIA UWANJANI

**Na Adam Fungawango**

SHABIKI wa Klabu ya Simba aliyetambuliwa kwa jina la Mohamed Salehe amefungiwa kutohudhuria mechi yoyote ile uwanjani kwa muda wa mwaka mmoja, kwa kosa la kuingia uwanjani wakati mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo dhidi ya Mashujaa FC ikichezwa.

**Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Machi 15, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Simba ilishinda mabao 2-0.**

Walinzi watatu wa klabu hiyo, 'Stewards', Kessy Mohamed, Mrisho Mindu na Mohamed Salmin, nao wamefungiwa kuingia uwanjani kwa miezi 12 kutokana na kosa la kushiriki katika tukio la shabiki wao Mohamed kuingia uwanjani wakati mchezo ukiendelea.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari ya Bodi ya Ligi, adhabu hiyo imetolewa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), katika kikao chake ilichokaa Machi 20, mwaka huu, ambapo pamoja na mambo mengine, ilipitia matukio mbalimbali ya ligi na kufanya maamuzi hayo ya mchezo huo namba 166.

Taarifa inaeleza kuwa Bodi ya Ligi inaendelea na uchunguzi kwa lengo la kufahamu wahusika wengine wa tukio hilo ambao hawakutambulika mara moja kwa ajili ya kuchukua hatua za kikanuni.

Adhabu hiyo imetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 47:2 ya Ligi Kuu kuhusu udhibiti wa klabu.

Pamoja na hilo, Klabu ya Simba pia imepigwa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la walinzi wake na shabiki kupanga njama na kufanikisha azma ya kuingia uwanjani na kufanya vitendo vinavyoashiria imani za kishirikina wakati wa mchezo huo, katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Taarifa imeeleza, mashabiki hao walionekana kupitia video fupi iliyosambaa mitandaoni na walijadiliana na mlinzi wa uwanjani kabla ya kuingia uwanjani na kufanya tukio hilo lililoleta taswira mbaya kwa Ligi ya Tanzania.

Bodi imesema, kwa mujibu wa kamati hiyo, adhabu hiyo ni kwa kuzingatia Kanuni ya 47:1 ya Ligi Kuu kuhusu Udhibiti wa Klabu.



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Kelvin John, akiwazidi ujanja mabeki wa Mongolia na kwenda kuifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 3-0 kwenye mechi ya Fifa Series 2024, iliyopigwa nchini Azerbaijan jana. **PICHA: TFF**

## Stars yaishushia hasira Mongolia

INATOKA UKURASA 24

anayecheza soka la kulipwa katika Klabu ya K.R.C. Genk ya Ubelgiji, baada ya kazi nzuri ya Ben Starkie aliyetokea benchini.

Ni kipindi ambacho Kocha Mkuu, Hemed Morocco, aliamua kumtoa kipa Kwesi Kawawa na kumuingiza Aboutwalib Mshery.

Sopu alipachika bao la pili dakika ya 61 kwa shuti kali la mbali, ambalo kipa wa Mongolia Tsenguun Khandaa pamoja na kuruka alishindwa kuuzuia.

Dismas, anayechezea Klabu ya Shakhtar Donetsk ya Ukraine, baada ya kukosa bao yeye na wavu dakika ya 70, alipotaka kufunga kwa madaha kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Kelvin, hatimaye alirekebisha makosa yake dakika tano baadaye alipopachika mpira wavuni, akiandika bao la tatu, kazi nzuri iliyofanywa na Sopu.

Katika kipindi hicho cha pili, Stars ilionekana kutawala soka zaidi kuliko cha kwanza, wapinzani wao wakionekana kuchoka na kukosa stamina kila dakika zilipokuwa zikisonga mbele.

Wamongolia walifanya mashambulizi machache sana langoni mwa Stars na muda mwingi mwa mchezo kipa alikuwa likizo.

Kuna wakati ilionekana kama Stars inacheza bonanza kiasi kwamba kama wachezaji wake wangekuwa makini wangefunga idadi kubwa ya mabao.

Stars ilicheza mechi hiyo ikiwa haina baadhi ya wachezaji kama Kibu Denis, Mohamed Hussein 'Tshabalala' wa Simba, Ibrahim Hamad 'Bacca', Mudathir Yahaya na Clement Mzize wa Yanga ambao walirejea nchini kuungana na timu zao ambazo wikiendi hii kila moja ina kibarua cha kucheza mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Michezo

Jumanne Machi 26, 2024

Nipashe



Alia Real kumzuia kucheza Olimpiki UKURASA 22

VINYOZI...



Wafungaji wa mabao ya Taifa Stars wakati ikishinda 3-0 dhidi ya Mongolia kwenye mechi ya Fifa Series 2024, Abdul Sopu (kushoto), Novatus Dismas na Kelvin John. Mechi hiyo ilipigwa nchini Azerbaijan jana. **PICHA: TFF**

# Stars yaishushia hasira Mongolia

**Na Adam Fungamwango**

MABAO matatu yaliyofungwa na Kelvin John, Abdul Suleiman Sopu na Novatus Dismas, jana yalitosha kwa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kushusha hasira zake za kupoteza mchezo wa kwanza dhidi ya Bulgaria kwenye mechi hizo za Fifa Series 2024 zilizopigwa nchini Azerbaijan.

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Dalga Arena, Stars ilishinda 3-0 na ingeweza kuondoka na ushindi hata wa mabao 8-0 kama wachezaji wake wangekuwa makini.

Katika mechi ya kwanza, Stars ilichapwa bao 1-0 dhidi ya timu ya Taifa ya Bulgaria kwenye uwanja huo.

Pamoja na kufunga mabao hayo, wachezaji Kelvin, Feisal Salum na Novatus ndiyo walioongoza kwa kukosa mabao mengi ya wazi. Mpaka dakika 45 za mwanzo, timu hizo zilikuwa hazijafungana, huku Stars ikionekana kutawala sehemu kubwa ya mchezo huo.

Stars ilianza kukosa mabao dakika ya 16, Kelvin 'alipotambaa' na mpira kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi iliyokosa muunganishaji, Fei Toto akishindwa kuuweka mpira wavuni licha ya kupata pasi murua kutoka kwa Kokola Charles.

Dakika ya 31, Kokola alimimina krosi ambaye Dismas alishindwa kuuweka mpira wavuni, na dakika moja kabla ya mapumziko shuti la Fei Toto aliyepenyezewa pasi na Kokola, liliwababatiza mabeki wa Mongolia na kurejea uwanjani.

Kipindi cha pili baada ya mabadiliko, Stars iliandika bao la kwanza dakika ya 48 kupitia kwa Kelvin

INAENDELEA UKURASA 23

# PACOME, AUCHO FITI KUIVAA MAMELODI

●●● Yao bado hatihati huku Kibwana naye akielezwa hajawa sawa kwa...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imetangaza hali ya wachezaji wake wote waliokuwa majeruhi, ikisema wachezaji wao, Pacome Zouzoua na Khalid Aucho, wako fiti kwa asilimia zaidi ya 80 na watacheza mechi ya robo fainali Jumamosi dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, ila bado kuna wasiwasi kuhusu beki wao Yao Kouassi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, pamoja na mambo mengine alizungumzia hali za majeruhi wa klabu hiyo, jambo ambalo limezua wasiwasi mkubwa kuelekea kwenye mechi ya kwanza ya robo fainali itakayochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**"Pacome wote ni mashahidi mlimuona alikuwa mmoja wa wachezaji waliokuwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Ivory Coast kikicheza dhidi ya Benin. Mchezaji kukaa benchi tu ina maana ni sehemu ya kikosi na angeweza kuingia muda wowote ambao kocha anahitaji, kwa maana hiyo wala haihitaji utaalam sana kujua kuwa yupo fiti.**

"Taarifa rasmi ya mawasiliano kati ya madaktari wetu na wale wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, wametuhakikisha kuwa amepona kwa zaidi ya asilimia 85 na utimamu wake wa mwili umeimarika kwa hiyo hakuna shaka kama kocha anataka kumtumia Jumamosi atafanya hivyo," alisema.

Kamwe pia amesema kiungo mkabaji wa timu hiyo, Aucho, naye yupo fiti kwa asilimia 80, huku beki Kouassi akiwa kwenye hati hati ya kuikosa mechi hiyo.

"Zawadi Mauya tayari ameshaanza mazoezi na kikosi, amepona kwa asilimia 100, Kibwana Shomari yupo asilimia 60 ya utimamu wake, anaendelea kufanya mazoezi ya peke yake, hajaanza mazoezi ya pamoja, Aucho, yupo tayari kwa asilimia 80 kwa kazi ya Jumamosi, Kouassi bado imesalia kuwa 50 kwa 50, anaweza kucheza au asicheze inategemea na maendeleo ya jeraha lake.

"Tunaomba Mungu kuwa hadi siku ya mchezo wachezaji hawa wote wawe salama na wamepona kabisa majeraha yao na tuweze kupata kikosi kamili ambacho Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, atakuwa na uwanja mpana wa kuwatumia wachezaji wake," alisema Kamwe.

INAENDELEA UKURASA 23



Pacome

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >